CHUO CHA BIBILIA

Walawi,

Hesabu, Kumbu Kumbu La Torati

Na Yoshua

KITABU CHA # 2

Sura ya 1

Kitabu cha Walawi

Watu wengi wanaoisoma Bibilia wao hukifikiria kitabu hiki cha Walawi kuwa ni kitabu kigumu mno. Wao hukitambua kama kitabu chenye kuchosha kwa maelezo sahihi kuhusu Hema la Ibada huko jangwani na katika theluthi ya tatu katika kitabu cha Kutoka. Wanapokifikia kitabu cha Walawi, wao hukata tamaa ya kuisoma Bibilia nzima.

Neno hili "Walawi" lamaanisha, "Yanayohusika nao Wana wa Lawi." Walawi walikuwa ni makuhani wa Kihebrania. Ili kukielewa kitabu cha Walawi, ni jambo la muhimu mno kwamba uweze kufahamu ile "Hema ibada," na ndogo huko jangwani ambapo hawa makuhani walikuwa nao usimamizi katika kuzitoa dhabihu, na matoleo pamoja nazo ibada zingine. Baadaye, Hekalu lake Sulemani, na ambalo lilikuwa nao urembo mkuu, lilikuwa limejengwa juu ya mfumo sawa nao ule wa kwanza wa lile Hema la Ibada ambalo Musa alikuwa ameamriwa kulijenga huko jangwani.

Jambo mojawapo lililo kuwa la kutambulikana kuhusu Hema lile ndogo la Ibada ni kwamba lilikuwa liwezekwa katikati ya kambi yao makabila kumi na mawali ya Israeli wakati wote walipokuwa wakizunguka na kuivuka ile jangwa kwa miaka arubaini. Kweli kwamba Hema la Ibada lilikuwa liwe katikati miongoni mwao kwenye kambi ilikuwa ni mfano wa jambo fulani. Amri ya kwanza ni ile ambayo ilinena kwamba Mungu alitakikana awe wa kwanza. Maandiko yatufundisha kwamba Mungu atakikana awe kina cha mambo yote maishani mwetu. Hili ladhihirishwa, au kuonyeshwa mfano, kwa kweli kwamba lile Hema la Ibada lilikuwa katikati ya kambi yao.

Labda jambo la muhimu mno tunaloweza kulitambua kutoka katika Hema La Ibada ni kweli kwamba Mungu kwa hakika, na kwa kweli alipata kuishi katika lile Hema La Ibada. Tunazidi kuelezwa kwamba wakati Musa alipomaliza kulijenga Hema lile la Ibada, uwepo pamoja nao utukufu wake Mungu ulishuka na kuijaza sehemu ile ya ndani ya Hema, ambayo ilifahamika kama Patakatifu pa patakatifu, ambao ni mfano bora kuhusu jinsi ambavyo Roho Mtakatifu anavyowajaza waamini katika siku ya leo.

Kama ambavyo wana wa Israel walivyo zidi kusafiri kupitia nyikani, wingu ambalo lilikuwa juu ya hema lilikuwa likuwaongoza wao. Wakati ambapo wingu liliposonga, wao pia walisonga pamoja nalo. Wakati wingu liliposimama, wao pia walisimama nalo. Na kwa njia hii, wingu lile liliwaongoza wao. Watu wangelisongea kwenye lile hema kwa ajili ya msamaha, Ibada, na kwa uongozi.

Ujenzi wa Hema

Hivi kwamba twafahamu sababu ya hema, hebu tusongelee karibu na kuutazama namna ya ujenzi wake. Hema hii ya Ibada ilikuwa na hua iliozungukia pande zote, na ilikuwa imejengwa na msokoto wa kamba iliyokuwa ikifanana na hema. Maeneo yaliokuwa yakizunguka lile hema yalikuwa yakifahamika kama nyuani. Baadaye, nyuani zile katika Hekalu lake Sulemani zilifanyika kuwa nayo maeneo makubwa (Hektari zaidi ya 5.5). Lakini katika Hema la kwanza la Ibada hazikuwa ni kubwa vile.

Kulikuwemo baadhi ya vyombo ambavyo vilikuwa ni vya muhimu mno katika Hema la Ibada. Ni muhimu kutambua kwamba vyombo vyote vilikuwa navyo vipini vya kushikilia. Hii ilikuwa ni ya muhimu kwa kuwa ilikuwa kwa sababu vilibidiwa kubebwa kote katika kuzurura kwao nyikani.

Chombo cha kwanza kilichokuwa mle nyuani, hapo tu baada ya kuingia malangoni, kiliitwa Madhabahu ya Shaba. Madhabahu haya yalifanana na jiko kuu la makaa.

Moto ulikuwa kwenye Madhabahu ya Shaba kwa wakati wote. Wakati mwenye dhambi alipokuja kwenye hema akiutafuta msamaha wa dhambi, angalikutana naye kuhani huko kwenye uani. Halafu yule mnyama aliyekuja pamoja naye angelichinjwa kulingana na maongozi yale waliyopewa Walawi. Baadaye, yule mnyama angeliwekwa juu ya Madhabahu yale ya Shaba. Huku yule mwenye dhambi akiwa ameketi kwenye malango ya uani. Naye kuhani angeliingiea kwenye sehemu ya hema hii. Baada yake kuhani kuiweka ile dhabihu juu ya Madhabahu ya Shaba, huku moshi wake ukipanda kumwelekea Mungu, kuhani alikielekea chombo kingine mle uani, ambacho kiliitwa Birika. Ilikuwa kama bakuli kuu la kuogea. Hapa ndipo ambapo ilimbidi kuhani kujisafisha kulingana na sherehe na kwa niaba yake mwenye dhambi, ambaye alibakie kule kwenye langoni uani.

Hema, lenyewe lilikuwa limefunikwa kote, na lilikuwa limegawanyishwa katika sehemu mbili. Sehemu ile ya nje ilikuwa ikifahamika kama Mahala Patakatifu. Kulikuwepo na pazia nzito iliyogawanyisha hapa mahala patakatifu kutokana na sehemu ile ya ndani, iliyoitwa Patakatifu pa Patakatifu. Hapa Patakatifu pa Patakatifu ndipo ambapo Mungu alikuwa akiketi. Pazia hili lilikuwa limejengwa kwa nyuzi zilizokuwa zenye nguvu mno. Msomi Myahudi anayeitwa Yosephus atueleza sisi kwamba vikundi vya farasi kadha havingeliweza kulipasua pazia hili hata kama lingelivutwa upande moja nao mwingine. Pazia lililokuwa katika hekalu lake Sulemani, ndilo lililokuwepo katika nyakati zake Yesu, na lilikuwa ni pazia kubwa mno lililofanana na lile ambalo huwa ndani ya majumba mengi ya sinema au ya michezo ya kuigiza kwa ukubwa wake.

Twaelezwa katika vitabu vya Injili kwamba wakati ule ambao Yesu alifariki msalabani, pazia lile, lililokuwepo kati ya mahala Patakatifu na pale Patakatifu pa Patakatifu, lilipasuka toka juu hadi chini (Tizama Marko 15:38). Huu ni mojawapo wa miujiza mikuu ya Bibilia, na ambao kwa wakati mwingi hautambulikani kamwe.

Kulikuwepo na vyombo vinne katika Hema ya Ibada. Baada ya kuoga na kujisafisha kufuatia sherehe pale kwenye birika ya kuogea, kuhani alikwenda katika sehemu ya kwanza iliyofunikwa mle hemani, au mahala Patakatifu.

Katika mkono wake wa kushoto kulikuwepo na Kinara cha taa. Kinara hiki cha taa kilikuwa ni cha muhimu mno. Kiliwakilisha ufunuo ambao Mungu alikuwa amewapa watu wake Mungu wakati ambapo aliwapa wao Neno la Mungu – na, kwa hakika, ufunuo huu uliwaonyesha wao jinsi ya kumwendea Mungu. Hivyo basi kuhani angeliabudu mbele ya kinara cha taa na kumshukuru Mungu kwa Ufunuo ambao Yeye alikuwa amewapa watu wake Mungu na yule mwenye dhambi ambaye bado alikuwa huko nje uani.

Katika mkono wake wa kulia, kulikuwa nayo meza ya wonyesho. Sababu yake ilikuwa ni ili kuwakumbusha wao makuhani mfano wa Mana, ambayo Mungu hutupa kila siku kwa ajili ya riziki yetu ya kila siku.

Mbele yake, karibu kabisa na pazia ambalo lilitenganisha na kuzuia Patakatifu pa Patakatifu, palikuwa na Madhabahu ya Uvumba. Hapa katika Madhabahu ya Uvumba, kuhani angelisimama na kuomba maombezi kwake yule mwenye dhambi aliyekuwa angali huko nje uani. Huyu kuhani angelifika hadi hapa tu, halafu angelirudi na kukutana naye mwenye dhambi mwingine na kuirudia ile ile taratibu kwa mara nyingine.

<u>Mara moja kwa mwaka, watu wote wangelikutana kwenye Hema la Ibada. Na katika kongamano hili, Kuhani mkuu angeliingia kwenye pazia hadi katika Patakatifu pa Patakatifu na kuitoa damu ya dhabihu kwa ajili ya dhambi yao wenye dhambi wote.</u>

Huku tukizidi kutizama hii Hema ndogo ya Ibada, twahitajika kutambua kwamba kila chombo kilichokuwepo ndani mwake kilikuwa ni mfano wake Yesu Kristo. Na kwa sababu hiyo basi, hebu tutizame kwa uangalifu zaidi kila kimoja kwa karibu zaidi.

Vyombo Vya Hemani

Madhabahu ya Shaba kwa hakika ya hubiri Injili ya Agano Jipya. Wanyama wote walitolewa kama sadaka katika Madhabahu ya Shaba, na dhabihu zote za wanyama zilitimilika wakati Yesu Kristo alipokufa juu ya msalaba. Madhabau haya ya Shaba yasema kwetu sisi, "Wewe hauwezi kumkaribia Mungu bila ya dhabihu. 'Bila ya kumwagika kwa damu hamna msamaha wa dhambi'" (Tizama Waebrania 9:22).

Chombo kile kinachofahamika kama birika au bakuli, pale ambapo yule kuhani alijisafisha kwa sherehe kabla ya ya kuingia Mahala Patakatifu, pa tuzungumzia kwetu sisi, yale ambayo Maandiko yasema katika mahala pengi: "Ni nani atakayepanda katika mlima wa Bwana? Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe," (Zaburi 24:3-4)

Ushirika pamoja naye Mungu ndilo lengo kuu katika Hema la Ibada. Na mambo yote yaelekea katika upande ule. Na katika Bibilia, ushirika naye Mungu wafananishwa wakati mwingi na maankuli. Birika lasema kwetu yale wakati mwingi mama wazazi wetu waliyotuambia sisi tukiwa wachanga, "Nawa mikono yako kabla ya kukila chakula." Jisafishe kabla ya kukila chakula, na kabla ya kuwa nao ushirika naye Mungu. Ni lazima unawe; ni lazima usafishwe. Huu ulikuwa ndio ujumbe kuhusu Birika au Bakuli.

Huku kuhani akiwa amesimama kwenye Kinara cha Taa cha Dhahabu, alikuwa akitambulisha kwamba Mungu alikuwa ndiye kina cha Kitabu hiki ambacho tunakifanyia ukaguzi katika uchambuzi wetu wa Bibilia. Yeye alikuwa akitambua kwamba Neno lake Mungu ndiyo nuru ya uongozi. Yeye alikuwa akimwambudu na kumshukuru Mungu kwa kumpatia mwenye dhambi aliyekuwa pale nje uani ufunuo wa jinsi ambavyo angeliupata wokovu na kumjia Mungu Mtakatifu katika Ibada.

Na kama tulivyo tambua hapo juu, mkate uliokuwa juu ya Meza ya Wonyesho ulikuwa ni mfano wa kweli kwamba Mungu angeliwapa riziki yao pamoja na kukutana nayo mahitaji ya watu wake. Ni wazi kwamba Mungu hatutaki sisi kupoteza mbali kweli kwamba yeye ndiye kina cha riziki yetu. Yeye atutaka sisi kumtumaini Yeye na kumtazamia Yeye kwa kila hitaji tulilo nalo, kimwili, kihisia, kiakili, na kiroho.

Jambo Lingine, hebu tutazame Madhabahu ya Uvumba. Huku kuhani akiwa amesimama kando ya madhabahu haya, yeye angelimwombea mwenye dhambi ambaye alikuwa amesimama huko nje uani kwenye lango. Na huku akifanya hivyo, Yeye alikuwa ni mfano wake Yesu Kristo, Kuhani wetu Mkuu, ambaye hutufanyia maombezi mbele ya Baba.

Kwa Ufupi

Kila kitu katika Hema ya Ibada kilikuwa ni kumhusu Yesu. Yeye ndiye Nuru ya ulimwengu, Yeye ndiye Mkate wa Uzima, Yeye ndiye dhabihu kamilifu. Yeye ndiye ambaye huja na kutuosha sisi katika birika. Kwa hakika ni Injili ya Yesu Kristo ambayo waiona katika Hema hili dogo la Ibada. Ni wakati tu ambapo unapofahamu Hema ya Ibada ndipo waweza kutumainia kukielewa kitabu cha Walawi kwa kuwa Walawi kilikuwa ni kitabu cha mwongozo na utaratibu ambao kuhani aliutumia katika Hema la Ibada. Je! Wamfahamu huyu Yesu ambaye anadhihirishwa katika Hema hili dogo takatifu?

Sura ya 2
Maskani Siku Ya Leo

Katika kitabu cha Mwanzo, twasoma ya kwamba wakati mwanadamu anapoitenda dhambi matokeo mabaya zaidi ni talaka – kutenganishwa – kati yake Mungu na mwanadamu.

Suluhisho kwa shida hii ya tangia hapo mwanzoni, ni upatanisho kwa talaka hiyo, kwa hakika ni ile ambayo ndiyo maana yake kuwepo kwa Bibilia – na hilo ndilo sababu kuu ambalo lahusu Maskani au Hema katika nyikani.

Na hivyo basi, ni kwa sababu gani katika siku ya leo sisi hatuifanyi dhabihu ya mnyama siku ya leo? Ni kwa sababu Mahitaji yake Mungu yamebadilika. Tutakapo kifikilia kitabu cha Waebrania tutakua nayo mengi ya kuyasema kuhusu haya. Lakini, kwa ufupi, Waebrania 9 yasema kwamba hili Hema la Ibada lilikuwa ni mfano wa maskani au hema nyingine ambayo ipo katika hali ya ubinguni. Hii maskani ya kimbinguni haikuundwa kwa vitu vya asilia ya dunia hii. Muundo wake ni wa kimbinguni, na ni vya kiroho. Maskani ambayo Mungu alimwambia Musa kuijenga kwa uhakika ni yenye kuonekana kwa macho ya kawaida, na kielelezo sahihi duniani kuhusu ya maskani iliyopo mbinguni na ya kiroho inayoelezwa katika Waebrania 9.

Kumbuka, wakati Yesu alipokufa juu ya msalaba, pazia katika Hekalu la Sulemani lilipasuka toka juu hadi chini. Kadhalika tilia maanani, kwamba mara moja kwa mwaka kuhani angeliingia katika Patakatifu pa Patakatifu, naye angelichukuwa damu ili kuzifunika dhambi za watu wote. Na katika hali ile ile, wakati Yesu alipokufa msalabani alifanyika kuwa yeye ni Kuhani Mkuu na huko mbinguni, akaupitia mfumo wa ibada ya maskani au hema ya kimbinguni. Katika Madhabahu ya Shaba kwenye maskani ya mbinguni, yeye aliutoa uhai wake kama timizo la mwisho kwa dhabihu zote za wanyama. Yeye alikwenda kwa birika, naye akaufanya usafishaji wa daima kuwezekana.

Kabla ya kifo chake Kristo, mwenye dhambi hangeliweza kumkaribia Mungu. ni kuhani peke yake ambaye angelimkaribia Mungu na kufanya maombezi kwa niaba yake mwenye dhambi. Lakini haya yote yaliondolewa wakati Yesu Kristo alipokufa juu ya msalaba. Wakati Yesu Kristo alipokufa msalabani, alikuwezesha wewe na mimi kukaribia mbele ya uwezo wake Mungu bila ya kipingamizi.

Tukio lingine lililo la muhimu kutokana nalo tendo hilo lake Kristo ni kwamba miili yetu imefanyika kuwa ni hekalu lake Mungu. Kwa kiini kamili, Paulo aliandika haya: “Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! Au hamjui ya kuwa yeye aliyeunganishwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja. ‘Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala nyinyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.” (1 Wakorintho 6:15-20) katika Wakolosai 1:27, Yeye atuambia sisi: “Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ya utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu;”

Kristo ndani mwenu ni muujiza. Hii ya maanisha kwamba uwepo wake Mungu waishi ndani mwenu; na pia hii ya maanisha kwamba unayo yale yote unayoyahitaji ili kuishi kwa njia ambayo Mungu amekuita wewe kupata kuishi.

Hebu sasa tufikirie kuhusu huu mfano wakuvutia kuhusu hema ya Ibada katika maisha yetu. Unapoamka asubuhi, ni shauku langu kwamba wewe unao wakati wa kimya mbele zake Mungu, wakati wa kuabudu, na wakati mbele ya uso wake Mungu kabla ya kuenda kwa shughuli nyingine za kilimwengu kwa siku ile. Wakati utakapo tenda hivyo, jaribu kufikiria njia yako ndani mwa Hema ya Ibada.

Hebu jifikirie ukisongelea hadi kwenye Madhabahu ya Shaba nawe utilie tumaini lako katika Habari Njema ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ndiye mwana kondoo wake Mungu

aliyekufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako. Na kama wewe haujamtumainia Kristo kwa msamaha wa dhambi zako, wa weza kufanya hivyo sasa. Na halafu mshukuru Mungu kwa msamaha katika msalaba wake Yesu, nawe uthibitishe ushawishi wako kwamba yeye alikuwa ndiye dhabihu kamili kwa dhambi zako.

Zidi kuendelea katika kujifikiria ukisongelea kwenye birika, ambapo wahitajika kusafisha mikono pamoja na miguu yako, mahala ambapo wahitaji utakaso wa kuendelea. Je! Yapo mambo katika maishani mwako ambayo ni machafu, na hayampendezi Mungu? Ungama haya kwake Mungu; yageukie mbali na upate kusafishwa. Halafu baadaye kwa njia ya usemi, karibia Mahala Patakatifu na usimame mbele ya Kinara cha Taa. Mshukuru Mungu kwa ufunuo; mshukuru Mungu kwa kuwa hakukuacha katika giza kuhusu uzima na wokovu. Mshukuru Mungu kwa Neno lake Mungu.

Endelea kujiona mwenyewe ukiwa umesimama mbele ya Meza ya Wonyesho, na umshukuru Yeye kwa kukutana na mahitaji yako yote. Mkiri Yeye kama kina kikuu cha kila kipande cha riziki na maali yote uliyonayo, na kwa kila njia ambayo mahitaji yako yanatimilizwa. Mkiri Yeye kama ndiye mwenye kukutana na mahitaji hayo, na ukiri hivyo kwa shukurani.

Huku ukizidi kufikiria kuhusu Madhabahu ya Uvumba, tafakari kuhusu mwujiza wa maombi. Nawe uuchukuwe wakati kwa kuomba kuhusu kila jambo katika mahitaji yako pamoja nazo changa moto zinazokukabili wewe kwa siku ile.

Unapoendela kutafakari kuhusu Patakatifu pa Patakatifu, hebu jambo hili na likupe wewe changa moto na ukumbusho kwamba kipo kitu kama uwepo wa Kiungu kutoka kwake Mungu. Kumbuka kwamba Roho wake Mungu yupo ndani mwetu na kwamba twaweza kuwepo katika uwepo wake Mungu po pote pale tulipo. Hatumhitaji kuhani ili kuenda mbele za uwepo wake Mungu kwa niaba yetu sisi. Na siyo lazima tuufatilie utaratibu ule uliokuwa katika Hema ya Ibada kwa kuwa wakati Kristo alipokufa juu ya msalaba, alituwezesha sisi kumwendea moja kwa moja hadi katika uwepo wake Mungu.

Yapo mafunzo mengi mno yatokanayo kutoka katika Hema huko Nyikani. Hili ndilo la muhimu mno: Ingali inawezekana kwake mwanaume au mwanamke mwenye dhambi kumkaribia Mungu Mtakatifu na kwa hakika kuingia katika uwepo Wake kupitia kwa njia mpya na yenye uhai ambayo iliwezekana kumpitia Yesu Kristo Bwana wetu.

Tunapotilia maanani kile ambacho kilimbidisha Mungu kutenda ili kuliwezesha jambo hili, waweza kudhania kwamba kungelikuwa nao msongamano mkuu kuelekea katika uwepo Wake. Lakini mbona hakutendeki hivyo? Je! Wewe umewahi kuwepo katika uwepo wake Mungu Mtakatifu? Yesu alitangaza hivi: “Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.” (Yohana 14:6) Tunauona huu msitari mkuu wa Injili mfano wake ukiwa katika Hema la Ibada. Mungu ataka kukutana nawe na kuyafanya maisha yako yawe Maskani au Hema lake.

Sura ya 3

Hali Ya Dhabihu

Na kwa kuwa sasa tunaomtizamo fulani kuhusu Hema ya Ibada, tupo tayari kukisoma hiki kitabu kidogo cha Walawi.

Kwa hakika kitabu hiki ni kitabu chepesi chenye utaratibu na muongozo kwao makuhani. Ni kitabu chenye mwongozo na utaratibu wa kinaga ubaga kuhusu kama jinsi ya kumchinja mnyama, na jinsi ya kufanya na matumbo yake yule mnyama na kila jambo. Hili labda silo la kutupa sisi shauku kuu kama jinsi ambavyo Zaburi 23 au I Wakorintho 13, lakini tafadhali usihisi kwamba hamna kweli za kiroho au matumizi ya kiroho ambayo

waweza kutunukiwa kutoka kwa Kitabu cha Walawi. Kitabu hiki kinacho kweli za kuvutia ndani mwake na ningelipenda kukuelekeza wewe katika sehemu fulani fulani katika bustani iliyopo katika kitabu hiki.

Sehemu Zake

Wahitajika kufahamu kwamba kitabu hiki cha mwongozo wao makuhani kimegawanywa katika sehemu kadha. Sura saba za kwanza za kitabu hiki zatilia mkazo juu ya dhabihu. Zinasema kwa ufasaha mno kile ambacho makuhani wahitajika kukitenda wanapotayarisha dhabihu hizi, lakini pia zatoa mwangaza kuhusu maana ya dhabihu hizi.

Katika sura ya Nane hadi sura ya kumi mkazo upo juu yao watumishi, au makuhani wenyewe. Mwongozo katika sehemu hii ni maelezo kuhusu yaliyohitajika na kutarajiwa kutoka kwao makuhani pamoja na kanuni walizohitajika kuzitimiza. Kwa njia ya kujifunza twaweza kutunukiwa mambo mengi mno yenye kuvutia kutoka katika sura hii.

Kina cha kitabu hiki chapatikana katika sura ile ya 11 hadi 22. Sehemu hii ya kitabu twaitaja kama “Utakaso”. Hema la Ibada pamoja nao makuhani ambao walikuwa wakihudumu mle walikuwa ndio tangazo lake Mungu kwa ulimwengu wote kwamba watu waliochaguliwa wake Mungu walikuwa ni watakatifu kwa kuwa Mungu wao alikuwa ni mtakatifu. Mkazo mkuu katika sura hizi ni kwamba hawa watu walichaguliwa ili wawe tofauti. Neno hili “Takatifu” lamaanisha “Kilicho mali yake Mungu”. Hawa makuhani walihitajika kuishi kana kwamba wao walikuwa kwa hakika wao ni mali yake Mungu.

Katika sura ya 23 hadi 25 kipo kile tunachokitaja kama “Huduma”. Zipo siku nyingi takatifu katika imani ya Kiyahudi, na waweza kuzipata katika maandiko ya vitabu vitano vya kwanza katika Bibilia. Na kwa kuwa hawa makuhani ndio walikuwa wenye kuhudumu katika siku hizi takatifu na katika hizi sherehe za kitaua, wao walihitaji maongozi kuhusu jinsi ya utaratibu wa kutumika.

Unapoijia hii sehemu ya Walawi, jiulize mwenyewe swala hili: Ni jambo gani ambalo Mungu aliwataka hawa makuhani kukumbuka wakati Mungu alipozianzilisha siku hizi takatifu, kama Pasaka? Halafu zidi kujiuliza swali hili: Ni kwa sababu gani Mungu aliwataka makuhani kukumbuka mambo haya?

Matimizo

Sura za mwisho za Kitabu hiki cha Walawi twazitaja kama “Kusalimu Amri”. Kitabu cha Walawi, Kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati, pamoja na Kitabu cha Yoshua vyamalizia kwa jumbe kuu za Matimizo. Vitabu hivi vyote vyamalizia kwa kuwahimiza watu wake Mungu mno ili wazitii sheria zake Mungu nao wawe watu watakatifu waliokuwa wameitwa kufanyika. Wao walikuwa wamekombolewa na walikuwa wameokolewa wawe watakatifu. Mahimizo katika mwisho wa Kitabu cha Walawi yafanya hizi sura za mwisho za kitabu hiki kuwa sura zenye uweza mkuu. Musa alikuwa amesema kwamba yeye alikuwa nacho kipingamizi katika usemi wake, au kwamba yeye hangeliweza kunena vyema, lakini hapa twamuona akiwa ni mwenye ufasaha mkuu katika mazungumzo yake.

Kujitolea, Kwa kibinafsi na Matumizi Yanayowezekana

Hebu tutizame baadhi ya baraka zilizopo katika kujitolea unazoweza kuzipata katika Walawi. Tutaanzia katika sehemu ya kwanza, “Dhabihu.”
Sura za kwanza saba za kitabu hiki zimetunukiwa kweli mojawapo zenye kuvutia mno kuhusu jinsi ambavyo makuhani walipewa mwongozo wa kuzitoa dhabihu kwake Mungu.

Kwa mfano, wakati mwenye dhambi alipokaribia kwenye Hema ya Ibada naye alitaka kuupokea msamaha, alikaribishwa kwenye lango naye kuhani. Huyu kuhani angelimpatia mwongozo kuhusu maana ya dhabihu ile ambayo huyu mwenye dhambi aliyoitaka kuwa kuitoa.

Pamoja na wajibu wao mwingine, makuhani walikuwa ni waalimu wao watu wake Mungu. Huku mwenye dhambi alipokuwa akiitoa dhabihu yake, kuhani alimwongaza yeye kuweka mikono yake juu ya kichwa chake yule mnyama. Wakati huyu mwenye dhambi alipotenda hivyo, yule mnyama alichukuwa nafasi yake. Dhambi zake zote yule mwenye dhambi zilihama juu ya kichwa chake yule mnyama. Kifo ambacho kingekuwa chake yule mwenye dhambi kulichukuliwa naye yule mnyama kwa niaba yake mwenye dhambi yule. Neno hili "Azazeli" latokana naye huyu mnyama na huu ndio uliokuwa umuhimu wa dhabihu hii. Wanatheolojia walitaja tendo hili kama kuwa "Upatanisho Kwa Niaba" wanapotumia hili katika mfano wenye kuvutia wa kifo chake Yesu Kristo juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi yetu.

Na pia unaposoma kitabu hiki, utavumbua kwamba kulikuwepo nazo nyakati ambazo taifa nzima lilikuwa limetenda dhambi na lazima kungelikuwepo na toba ya kitaifa. Walipotambua yale waliokuwa wameyatenda, iliwabidi kumtoa fahali mchanga kama dhabihu ya dhambi. Iliwabidi kumleta katika Hema, ambapo viongozi wa taifa wangelimwekelea mikono yao juu ya kichwa chake yule mnyama na halafu kumchinja mbele yake Mungu. Na halafu wangeliifuata taratibu ile ile kama jinsi ambavyo wangelitenda katika dhabihu ya kawaida ya dhambi. Katika njia hii, makuhani walikuwa wakiufanya upatanisho kwa ajili ya taifa lote. Je! Si hili ni jambo jema katika kuhusika kwenye ujuzi huu kama taifa nzima katika siku ya leo? Toba ya taifa nzima kwa ajili ya dhambi ya taifa nzima itakuwa ni tukio jema katika taifa lo lote lile. Tukio hili limeelezwa katika Kitabu cha Walawi.

Hawa makuhani iliwabidi wawe ni watu wenye kupakwa mafuta; hii ni kusema kwamba, iliwabidi wawe ni watu ambao waliongozwa naye Roho Mtakatifu. Ili kulieleza jambo hili, damu kutoka kwa dhabihu zile ilipakwa katika sikio na mikono na vidole vikuu vya miguuni vyao makuhani. Huu ulikuwa ni ujumbe kwake kuhani, "Wahitajika kuwa mtu mtakatifu. Utawaongoza watu katika kuwa watakatifu. Yale yote utakayoyasikia, yale yote utakayoyagusa au kuyatenda kwa mikono yako, na kila mahala ambapo utakapokwenda upakwe mafuta na kuongozwa naye Roho Mtakatifu."

Katika Kitabu cha Walawi, utakumbana pia nao mfano wenye kuvutia kuhusu kile tunachomaanisha tunaposema kwamba Musa aliandika kuhusu Yesu wakati Musa alipoviandika Vitabu vya Sheria. Katika Agano Jipya, wakati Yesu alipo alipo mponya mwenye ukoma, yeye wakati wote alisema kwake yule mkoma aliyeponywa, "Nenda na kujionyesha kwake kuhani." Ni kwa sababu gani Yeye alitenda hivyo? Kwa sababu, katika kitabu cha Walawi, utatambua kwamba kuhani walikuwa wamepewa huo mwongozo.

Unaposoma sura ya mwisho ya Kitabu cha Walawi, utapata sehemu nyingi zenye mahubiri mengi yenye kuvutia kwa ibada ya kibinafsi yake Musa. Kwa mfano, yeye amkariri Mungu kama akisema, "Kama mkienda katika amri zangu, nitawapeni nyinyi mvua, mavuno mema, miti yenu itakuwa yenye matunda mengi, zabibu zenu zitaendelea kuzaa hadi kufikia wakati wa kupanda tena. Mtakula na kushiba na kuishi na amani katika nchi ambayo nitawapeni nyinyi na mtakuwa nao usingizi usio na hofu. Mtawafukuzeni maadui wenu nao wataanguka chini kwa upanga wenu.

Watano miongoni mwenu watawafukuza mia moja na mia moja miongoni mwenu watawafukuza elfu kumi. Mtawashinda maadui wenu wote. Nitatembea kati yenu na kuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu Wangu." (Walawi 26: 3-12)

Utavumbua pia katika kitabu cha Walawi kwamba yapo baadhi ya mambo yaliyokatazwa, kama vile ulawiti (Mwanamume/mwanamke kufanya ngono na mwanamume/mwanamke mwingine). Ulawiti hauambatani katika mpango wake Mungu katika kuunganisha watu nao wazazi ambao huwazaa watu ambao hufanyika washirika na wazazi. Ulawiti umeharamishwa kwa kuwa karamu ya matokeo yake siyo mema. Musa anena bila ya kuficha cho chote kile. Yeye auhukumu ulawiti , kwa lugha nzito. Katika kitabu cha Walawi, Musa pia ahukumu uchawi, upigaji ramli, ubashiri, pamoja na mambo mengine mengi. Sheria zake Musa zilikuwa zenye uzito mkuu kwa kuwa watu wakiyahudi walitakikana kuwa watu watakatifu. Utakatifu ndilo tukio ambalo Mungu ataka kutufundisha sisi watu wake katika Kitabu cha Walawi.

Natumainia kwamba utangulizi huu pamoja na ukaguzi wa Kitabu hiki cha Walawi utakuwezesha wewe kukisoma kitabu cha Walawi kibinafsi na ubarikiwe kwa kufanya hivyo. Kumbuka, kitabu cha Walawi kilikuwa ni mwongozo kwao makuhani uliowaonyesha wao jinsi ya kupakwa mafuta, na kuwa watu watakatifu wake Mungu ambao wangeliwafunza watu wake Mungu jinsi ya kuwa watakatifu. "Iweni watakatifu, kwa kuwa Mimi ni mtakatifu, asema Bwana" – huu ndio ujumbe wa kitabu cha Walawi kwako na kwangu mimi.

Kitabu Cha Hesabu

Sura ya Nne
Kiwango Cha Uamuzi

Kitabu hiki cha Hesabu cha endeleza hadithi ambayo chanzo chake kipo katika Kitabu cha Mwanzo, huku mfumo wake ukipitia katika Kitabu cha Kutoka, na kwa kitambo kidogo kukatizwa wakati Mungu alipompa Musa kitabu cha mipangilio na maelezo kuhusu ujenzi wa Hema katika Nyikani.

Wakati wana wa Israeli walipo kombolewa kwa njia ya mwujiza kutoka utumwani katika nchi ya Misri, ilikuwa kwamba wavuke nyikani na kuingia katika nchi ya ahadi ya Kanaani. Kitabu cha Hesabu chatueleza kwamba wao hawakusafiri moja kwa moja kutoka Misri hadi Kanaani. Wao walizunguka katika miviringo huko nyikani kwa miaka arobaini.

Vivyo hivyo wengi miongoni mwa waamini katika siku ya leo hufanya haya haya. Wao wamekombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi zao kwa damu yake Kristo, hali wao hawaishi jinsi ambavyo Mungu alivyowaumbia pamoja na kuwaumba upya wapate kuishi. Wao wamekandamizwa, wenye kuchoshwa, wenye kujitakia makubwa, na wasiotosheleka. Wao hawajapata kuingia katika "Nchi ya Ahadi." Katika dhamana ile ya uzima ambayo Agano Jipya lautaja kama "Uzima wa Milele". (Yohana 3:15) Yesu akasema, "Nilikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." (Yohana 10:10) Agano Jipya lautaja uzima huu, kama udhamani wa "Uzima wa Milele".

Nchi ya Ahadi ya Kanaani ni mfano wa picha iliopo katika Agano Jipya ya dhamana ya kimaisha yake mwamini aliye okolewa aupate ujuzi huo. Badala yake, kwa mara nyingi wao huzunguka zunguka katika miviringo ya kutoamini, kukatatamaa, na kuchanganyikiwa. Kitabu cha Hesabu chatufundisha sisi somo hilo kwa mfano katika kunakili sura hii katika historia yao watu wa Kiyahudi.

Kuagamia kwa Kizazi

Kitabu hiki chapata jina lake kutokana na kweli kwamba Waebrania walipata kufanyiwa hesabu kwa mara mbili. Kulikuwapo nayo hesabu ya watu iliyofanyika katika sura tatu za kwanza za kitabu, na hesabu nyingine kutendeka katika sura ile ya ishirini na sita. Katikati ya hesabu ya kwanza na ile ya pili waweza kuona kuangamia kwa kizazi kizima.

Kwa sababu ya ukosefu wa imani, Mungu aliwaambia wana wa Israeli: “Mtaangamia jangwani. Hamna hata mmoja wenu aliye mwenye umri wa zaidi ya miaka ishirini, ambaye aliye nung’unika kinyume changu, atakaye ingia katika Nchi ya Ahadi. Ni Kalebu na Yoshua peke yao watakao ruhusiwa kuingia ndani mwake. Mlisema kwamba wana wenu watafanyika kuwa watumwa wa nchi hiyo. Badala yake, nitawafikisha salama katika nchi hiyo nao watakirithi kile mlichokidharau nyinyi. Lakini nyinyi, mizoga ya miili yenu itaanguka katika jangwani, nanyi mtazungukazunguka humu jangwani kwa miaka arobaini. Na kwa njia hii mtalipia kutokuamini kwenu hadi aliye wa mwisho miongoni mwenu atakapo anguka huko jangwani. Nitawafundisha nyinyi maana yake kunikataa mimi. Kila mmoja wenu ataangamia katika jangwa hili.” (Hesabu 14:34-36)

Huku wana wa Israeli wakizurura huko jangwani, Mungu kwa mara nyingi alijaribu kuthibitisha kwao kwamba Yeye alikuwa pamoja nao. Ili kuwapa msingi kwa imani yao, yeye aliitenda miujiza kwa ajili yao. Na kwa njia hii, alijaribu kuwapa wao imani ili kuamini kwamba wangeliweza kuvuka mto wa Yordani na kuivamia Nchi ya Kanaani.

Badala yake, wao walitoka Misri, wakavuka Bahari ya Shamu, wakapitia chini ya Mlima Sinai huko Kadesh Barnea, halafu kuuzunguka ule mlima kwa miaka arobaini. Tunaelezwa katika kitabu cha Kumbu Kumbu la Torati kwamba yachukua muda wa siku kumi na moja tu kusafiri kutoka Misri hadi Kanaani. (Kumbu Kumbu La Torati 1:2)

Katika jangwani, kwa mara kumi, Mungu aliitenda miujiza ya kushangaza ili kuijenga imani yao, lakini wao walizidi kuzunguka zunguka katika miviringo. Na kwa mara nyingi wao walitenda dhambi mbovu mno hivi kwamba ilimbidi Musa kuwa ni nabii na kuhani. Yeye angelipanda juu ya Mlima Sinai kama kuhani wao na kufanya maombezi kwa niaba yao kwake Mungu. Na kama kuhani wao kwa hakika aliyafanya maombi, “Tafadhali Ee Mungu wasamehe, tafadhali wasamehe wao.” Haya yalitukia kwa mara kumi na kwa mara kumi Mungu aliwasamehe wao. (Hesabu 14:22)

Kutoka katika Mlima Sinai, Musa aliomba, akimwuliza Mungu kuonyesha subira kwa kuzisamehe dhambi zao wana wa Israeli. Bwana aliwasamehe wao kama jinsi ambavyo Musa alivyomwomba, lakini akasema, “Ni kwa muda gani nitalivumilia kongamano hili ambalo lanung’unika kinyume changu? Nimeyasikia manung’uniko yao wana wa Israeli, ambayo wanayafanya kinyume changu. Waambie hivi, “Kama mimi niishivyo,’ asema Bwana, ‘Kama jinsi ambavyo mmesema mbele ya masikio yangu vivyo hivyo nitawatendea nyinyi; mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili, hata nyote miongoni mwenu mliohesabiwa, kulingana na miaka yenu tokea miaka Ishirini hadi kuendelea, walionung’unika kinyume changu mimi.” (Hesabu 14:27-29)

Je! Kulikuwepo nayo huzuni kubwa mno ya namna gani kote katika kambi, wakati ambapo Musa alipowapasha watu maneno yake Mungu! Wao walikuwa wamearauka asubuhi na mapema na kuanza kusafiri kuelekea katika Nchi ya Ahadi. Wao walifahamu kwamba walikuwa wametenda dhambi, lakini walikuwa tayari kuingia katika Nchi ambayo Bwana alikuwa amewaahidi wao. Lakini Musa akawaambia wao kwamba walikuwa

wamechelewa. Kwa kuwa wao walikuwa hawamo pamoja naye Mungu, naye alikuwa ameondoka kutoka kwao.

Kipande hiki cha historia yenye mfano chatueleza kitu fulani kuhusu uhusiano wetu naye Mungu. Yeye aliwasamehe wana wa Israeli, lakini dhambi yao ilimfanya kuwa nao uchungu mwingi. Na kwa njia ile ile, kipo kitu cha zaidi katika maisha yetu ndani kwa Kristo kuliko kusamehewa. Sisi tumeumbwa, na kuumbwa tena kupitia wokovu wetu, kumtukuza Mungu kwa kumtumikia Yeye na kuingia katika kila kitu ambacho ametupangia sisi. Bibilia yasema ipo sababu kwa wokovu wetu; ujuzi huu wa taifa la Israeli katika kuzunguka-zunguka jangwani na bila ya kuingia katika Kanaani ni dhihirisho ya kweli kuu kwamba yawezekana kwetu sisi kuikosa sababu ya wokovu wetu katika maisha haya.

Kiwango Cha Uamuzi

Wakati rubani wa ndege kuu anapoishukisha ndege chini kati ardhi, kwa mfano kama ile inayoitwa Concorde, Jumbo 747 yenye kuwabeba abiria wengi, yeye hufikia kiwango kile ambacho hawezi kughairi kushuka kwake na ambapo inambidi yeye kulazimika kushuka. Hii inatajwa kama kiwango ambacho mtu hawezi kurudi nyuma, au “Kiwango cha Uamuzi”. Kwa hakika Mungu ni mwenye subira nyingi na mwenye rehema kuu. Lakini, katika sura ile ya kumi na nne ya Kitabu cha Hesabu yatueleza kile tunachoweza kukitaja kama, “Kwango cha Uamuzi” katika safari yetu ya imani. Kipo kiwango katika kutembea kwetu naye Mungu ambapo twaweza kuufanya uamuzi kana kwamba twaweza, aitha kuyatenda mapenzi yake Mungu au tukatae kuyatenda mapenzi yake Mungu katika maisha yetu.

Hata ingawa Mungu atayafanya yale yote awezayo kuyafanya ile kutuwezesha sisi kuyaona mapenzi yake na kuyatenda, Yeye hupafikia mahala pamoja nasi ambapo yeye hutuachilia sisi kuyatenda mapenzi yetu, na kumtafuta mtu mwingine ile kukitenda kile ambacho yeye ataka kukitenda kutupitia sisi. Wakati Mungu anapogeuka kinyume chetu kwa sababu sisi twaufanya moyo wetu kuwa mgumu kwa kuyatenda mapenzi yake, sisi hukumbana nayo dhiki ya upotevu mwingi, kwa kuwa sisi hulikosa kusudi letu la wokovu katika maisha haya. Sisi kwa hakika hatuupotezi wokovu wetu, ila sisi twaipoteza fursa ya kutimiliza kusudi lile katika maisha haya, na ambalo Mungu ametufanyia wokovu kwalo. (Waefeso 2:8-10)

Baadhi ya misitari yenye huzuni kuu katika sura hii kuu ya kumi na nne katika kitabu cha Hesabu ni misitari ile ambapo Musa aliwaambia wao, “Mmechelewa kwa wakati huu! Vueni silaha zenu! Mmemwacha Mungu naye Mungu pia amewaacha nyinyi!”

Kipo kitu kama Mema, yenye kukubalika, na matimilifu mapenzi yake Mungu katika kila mmoja ya maisha yetu. Kitabu cha Hesabu ni kuhusu kuyatenda mapenzi yake Mungu katika maisha yetu. Unapo Kisoma Kitabu cha Hesabu sura ile ya Kumi na nne, hebu tizama pale picha ya kiwango cha uamuzi ambapo sote sisi huufanya uamuzi ambao labda tutakwenda kuyafanya mapenzi yake Mungu au tutadinda kuyatimiliza mapenzi yake Mungu katika maisha yetu. Haujachelewa mno katika kuufanya uamuzi kana kwamba hatutazungu-zunguka katika miviringo tena bali tuvamie na kumiliki “Kanaani” ambayo Mungu ametuandalia sisi.

Sura ya Tano

Mifano Yenye Kuvutia

Kitabu cha Hesabu kimejawa na mifano yenye uwezo mkuu na mafumbo. Mtume Paulo alitupatia ufunguo katika kulifanya neno lake Mungu kutimilika katika maisha yetu na hadithi zilizomo katika historia hii ya Bibilia kuwa sehemu ya maisha yetu. Wakati alipoandika hivi: “Haya yote yaliwatokea wao kwa ajili ya kuwa mfano kwetu na yaliandikwa kama maonyo kwenu nyinyi na kwangu mimi na ambao miisho ya ulimwengu imetujia sisi.” (1 Wakorintho 10:11) hii yamaanisha twahitajika kutafuta mifano nayo maonyo wakati tunapo soma hadithi za historia katika Maandiko.

Neno ambalo Paulo alilolitumia kwa “Mifano” ni neno ambalo laweza kufasiriwa kama “Namna” au, “somo dogo lenye mfano sawa na ile yenye kufundishwa” au “mafumbo”. Tunaposema kwamba kitabu hiki kimejawa na mafumbo, sisi hatumaanishi kwamba yaliyotukia humo si ya kweli kihistoria. Fumbo ni hadithi au tukio ambalo lenye maana kuu ambayo hutupa maongozi sisi ya kiroho au kitabia.

Wingu La Uongozi

Vifungu vya kufungia katika Kitabu cha Kutoka twasoma wakati ambalo Hema katika njangwani, au Hema la Ibada, lilipomalizika kujengwa na kuinuliwa juu, mwujiza mkuu ulitukia pale. Baadaye, Hekalu lake Sulemani lilijengwa kulingana nao mfumo ule ule wenye maelezo sahihi ambayo Mungu alikuwa amempatia Musa kwa ajili ya ujenzi wa Hema ya Ibada ya huko jangwani. Hekalu lake Sulemani lilikuwa ni jengo dhabiti na hekalu la Ibada na ujenzi wake ulikuwa wenye utukufu na dhamana isiyo na kipimo. Wakati hekalu hilo lilipowekwa wakfu, Roho wake Mungu, kama Wingu, pia alishuka na kulijaza Hekalu lake Sulemani hivi kwamba makuhani walikimbia kutoka nje ya hekalu lile. (1 Wafalme 8:10,11

Wakati Musa alipomtii Mungu na kulijenga Hema jangwani ya ibada, twasoma kwamba mwujiza mkuu ulitendeka katika mahala pale: “Siku ile ambayo Hema ilipoinuliwa, wingu likaifunika. Na hapo jioni wingu lile likageuka na kuonekana kama moto na kubaki hivyo usiku kucha. Na iliendelea kuwa hivyo, wingu la mchana lilibadilika na kuwa wingu la moto usiku. Wakati wingu lilipoinuka, watu wa Israeli nao walianza safari yao hadi ambapo wingu hilo liliposimama na wao kupiga kambi pale.

“Wana wa Israeli walimfuata Roho wake Mungu katika mfano wa wingu kote kati jangwani. Na kwa njia hii wao walisafiri kulingana nayo amri yake Bwana na kusimama pale ambapo yeye alipowaambia kufanya hivyo, na wao kudumu pale kulingana na jinsi ambavyo wingu lilivyo dumu pale. Kama wingu lile lilidumu kwa muda mrefu na wao pia walidumu pale kwa muda mrefu pia. Na kama lilidumu kwa siku chache, na wao pia walidumu kwa siku chache. Wakati wingu lilipo safiri, nao watu waliifunga kambi na kulifuata wingu lile. Na kama wingu lile lili dumu katika hema kwa siku mbili, miezi miwili, au mwaka, na kwa jinsi hiyo hiyo ndivyo wao walivyo dumu wana wa Israeli mahala pale. Punde tu wingu liliposafiri na wao pia walisafiri. Na hivyo ndivyo ilivyo kuwa kama wamepiga kambi, au kusafiri, kulingana nayo amri yake Bwana.” (Hesabu 9)

Hii ni hadithi yenye kuvutia kuhusu muujiza huu wa uongozi wa kiuungu, muujiza wa kazi ya Roho Mtakatifu ndani mwetu, na upako wa roho mtakatifu juu yetu. Baadaye, katika Agano Jipya, Hema hiyo ya Ibada yafanyika kuwa ni picha ya miili yetu, ambayo ilifanyika kuwa ni hekalu ambalo Roho Mtakatifu anaishi na kutenda muujiza wake wa kutufanya upya. Roho Mtakatifu hutupaka mafuta sisi, na kuishi ndani mwetu, na kutujaza

sisi kama jinsi ambavyo alivyofanyaa katika Hema ya Ibada na katika Hekalu lake Sulemani.

Labda waweza kuliuliza swala hili, “Ikiwa wingu hili liliwaongoza wana wa Israeli, na wao kwa utiifu wakalifuata, mbona wingu hilo halikuwaongoza moja kwa moja kupitia jangwani, na kuuvuka mto Yordani hadi katika Nchi ya Ahadi? Ilikuwaje kwamba wao waliufuata mwongozo wake Mungu na bado walikuwa wakizunguka-zunguka katika miviringo?”

Kuna kweli ya muhimu mno mahala hapa. Mungu humpa kiumbe kile alichokiumba uhuru wa uchaguzi. Hii ni picha mojawapo ya njia muhimu ambayo Mungu alivyo muumba mwanadamu katika mfano wake Mungu. Yeye hawezi kuuvunja uhuru wetu wa uchaguzi. Kama ikiwa tunayo imani ya kuamini na kukiri baraka zote zake Mungu alizonazo kwa ajili yetu sisi na kukubali mapenzi yake yaliyo mema na makamilifu katika maisha yetu, hapo ndipo atakapo tuongoza sisi katika Nchi yetu ya Ahadi ya kiroho. Yeye aweza kuziweka baraka juu yetu na kutuongoza sisi katika kina na moyo wa mapenzi Yake katika maisha yetu.

Lakini, kama hatuamini, kwa hakika hatutaigundua nchi yetu ya kiroho ya Ahadi. Yeye alitufanya sisi kuwa viumbe vyenye uchaguzi na hivyo basi ipo namna ambayo kwake yeye hawezi kutulazimisha sisi kutenda lolote lile. Mungu aweza kutuegemea sisi kama jinsi ya ndovu. Yeye aweza kutupatia ahadi nyingi ambazo hatuwezi kuzikataa. Mara nyingine, tunapozingatia chaguzi zetu, kitu kilicho cha maana kuu kwetu kitakuwa ni kwetu sisi kujisalimisha amri kwake Yeye na kuyatenda mapenzi yake.

Katika Agano Jipya, kwenye Kitabu cha Waebrania sura ya tatu na ile ya nne, sisi twaelezwa kwamba wao hawakuingia katika Nchi ya Ahadi kwa sababu ya kutoamini kwao. Haya ndiyo twaweza kujifunza kutoka kwa wingu na moto ambao haukuwaongoza watu moja kwa moja kupitia jangwani hadi katika Nchi ya Ahadi.

Nini Hiki?

Kweli nyingine ambayo twaipata katika kitabu cha Hesabu ni kuhusu ile hadithi ya nyama na Mana. Mungu kwa njia ya muujiza aliwalisha watu wake kwa Mana. Mana katika lugha ya Kiebrania yamaanisha, “Nini Hiki?” hawakukubaliana kilikuwa ni kitu gani, na hivyo basi wakakiita “Nini Hiki?” Mungu aliwalisha wao kwa “Nini hiki?” kwa miaka arobaini.

Tunaelezwa kwamba watu wake Mungu waliendelea kunung’unika kwake Musa. Hesabu 11:4-6 yasema: “Halafu Wamisri walioambatana pamoja nao walianza kutamani vitu vyema vya Misri.” Wapo watu wengine walioambatana nao wana wa Israeli mbali na Wayuhudi wenyewe. Wao walikuwa ni watu wamataifa, kama vile Waethiopia na Wamisri, walioambatana nao. Wamisri walitamani vitu vyema vya Misri. Lipo somo kwetu sisi katika hili. Yasema, “jambo hili liliwaongeza tamaa wana wa Israeli nao wakalia. Wakisema, ‘N’nani atakayetupa nyama tule. Angalau mtu angelitupa sisi samaki na tamutamu tuliyoifurahia huko Misri?’” (Hesabu 11:4-6)

Katika mazingara haya, Misri ni mfano wa maisha yetu ya kale ya dhambi katika ulimwengu. Wakati ambapo mtu ambaye amekombolewa kutoka “Misri” anageuka na kusema, “Nakutamani Misri,” hiki ni kiini cha kumhuzunisha Mungu. Mungu amwambia Musa haya katika kifungu hichi, “waambie watu kujitakasa wenyewe, kwa kuwa kesho wao wataipata nyama. Waambie kwamba Mungu amekisikia kilio chao na kuyaona machozi yao kuhusu yale waliyoyaacha huko Misri.” Huu ndio mwelekeo; na wala siyo ile nyama. Mungu asema atawapatia nyama hadi iwatoke kwenye pua zao. Mungu alisema,

“Mmemkataa Bwana, nanyi mkailiia Misri.” Huu ndio uliokuwa umuhimu wao. Baada ya kuwaletea wao nyama pia aliwatumia wao mapigo ya tauni. Yeye alitenda hivyo kwa kuwa hawa watu walikuwa wametamani nyama pamoja na Misri.

Maandiko yasema kwamba Mungu yeye atatupatia sisi tamaa za mioyo yetu. Hii ni faraja kuu, lakini pia ni changa moto kubwa. Je! Tamaa za moyo wako ni za mambo ya kiroho au tamaa za moyo wako ni za Misri?

Mungu aliwapa walichomtaka Akawakondesha roho zao. (Zaburi 106:15). Hili hutendeka na hivi ndivyo hutukia kwao watu wengi wenye kukiri kuwa waamini. Sisi tu viumbe vya uchaguzi. Twaweza kukipata kile tunachokichagua. Tunapo chagua Kitunguu na kile Kitunguu saumu kutoka Misri, Mungu atakutana nayo mahitaji Yetu, lakini pia atazikondesha roho zetu. Mfano huu wenye kuvutia ni changa moto kwetu kuhusu swali ambalo Mungu alilolifungua majadiliano nasi katika bustani la Edeni: “Upo wapi?” Je! Wewe ungalipo huko Misri? Je! Wewe upo katika Nchi ya Ahadi? Je! Wewe waranda-randa kote kote katika miviringo kati ya Misri na Kanaani? Je! Wewe upo Kanaani, lakini wavitamani vitu vya Misri?

Wapelelezi (Sura ya 13)

Tukio moja hili ni kuhusu jinsi ambavyo wana wa Israeli walivyo watuma wapelelezi kumi na wawili huko Kanaani. Wapelelezi waliambiwa wafanye upelelezi katika Nchi ya Kanaani ili kuona kama miji ya huko ilikuwa ime lindwa au la. Na pia walitakikana kufahamu jinsi watu wa nchi ile walivyo kuwa (Wengi au wachache, wanyonge au wenye nguvu) na kufahamu njinsi ambavyo itakavyo kuwa vigumu kuwa shinda na kuwatiisha.

Wakati wale wapelelezi kumi na wawili waliporudi, wao walizungumza mengi kuhusu rotuba na mazao ya Nchi ya Ahadi. Wao walikuja wamebeba furushi la zabibu lililokuwa kubwa mno hivi kwamba iliwabidi watu wawili kulibeba furushi lile kwa fimbo yenye kushikwa nao watu wawili mwishi moja na mwingine. Na pia waliwataja wakaazi wa nchi ile kama Majitu, shujaa wa vita, watu wenye misuli mikubwa, na kwamba miji ya Kanaani ilikuwa yenye ulinzi mkuu pamoja na kuta kubwa ambazo vyumba vilijengwa juu ya kuta zile.

Kumi miongoni mwa wapelezi kumi na wawili walikuwa ni watu stadi na maarufu katika elimu ya “Majitu”. Na kama jinsi wimbo moja wa kale wa kiroho ulivyo eleza: “Wingine waliwaona Majitu. Lakini Kalebu alimuona Bwana!” Mtu fulani alitunukiwa kutambua kwamba hawa wapelelezi kumi na wawili walikuwa kama kundi la kawaida lao wazee viongozi, shemasi, na wanachama wa baraza la uongozi kanisani. Wawili ni wenye imani ya kuvamia Kanaani, nao wale Kumi ni wenye ustadi katika elimu ya “Majitu” wenye kutilia mkazo katika yaliyo magumu.

Kalebu alifahamu ustadi na nguvu za ngome zilizopo katika miji ya Kanaani, lakini yeye hakuwa nayo hofu. “Kalebu aliwatia watu moyo alipokuwa amesimama mbele zake Musa. ‘Hebu twende huko mara moja na kuinyakua kwa kuwa twaweza kuitiisha nchi hiyo.’” (Hesabu 13:29-31) Mungu alivutiwa mno nayo imani yao hawa watu wawili, Kalebu na Yoshua hivi kwamba alikuwa tayari kuwapa wao fursa hali kuachana nalo taifa nzima la watu kati ya Laki Kumi na Laki Thelathini au Milioni moja na Milioni tatu. Akasema, “nyinyi nyote mtaanguka na kuangamia jangwani, nami nitawapeleka hawa watu wawili, Kalebu na Yoshua, pamoja nami hadi katika Nchi ya Ahadi kwa sababu wao waliniamini mimi na kunifuata mimi kwa mioyo yao yote.” Mungu huidhamini imani mno. Watu wawili wenye imani ni wenye dhamana kuu kwake Yeye kuliko halaiki za mamilioni yao watu wasio na imani.

Kipo kitu cha kuvutia katika hadithi hii na tutakachokifuatiliwa hapo baadaye. Mwishowe walipovuka Yordani miaka arobaini na mitano baadaye (Yoshua 14), wana wa Israeli walipofika katika mji wa Hebroni. Kalebu aliuona mji wa Hebroni kana kwamba ulikuwa ndio mji mkuu aliowahi kupata kuuona. Yeye aliamwamini Mungu angeliwapa Israeli uwezo wa kuivamia na kutiisha Hebroni. Musa alivutiwa mno nayo imani yake Kalebu hivi kwamba akamwahidi kuwa wakati wana wa Israeli watakapo uteka mji huo wa Hebroni kwa hakika, mji ule utakuwa ni wake Kalebu.

Baada ya kuzunguka-zunguka huko jangwani kwa muda wa mia arobaini, Kalebu alikwenda moja hadi kwake Yoshua, aliyekuwa ndiye kiongozi baada ya kufa kwake Musa na kumkubusha maneno yake Musa. Kalebu alikuwa mwenye umri wa miaka themanini na mitano, lakini alifahamu kwa msaada wake Mungu angeliinyakua Hebroni.

Yoshua alimpatia Kalebu mji wa Hebroni ili auteke na kuunyakua. Wakati wana wa Waisraeli wengine walipokuwa huko jangwani wakinung'unika mno hivi kwamba Mungu akawatuma nyoka kuwaangamiza wao, Kalebu hakufanyika sehemu ya kunung'unika kwao. Yeye alitilia mkazo na kuyaelekeza macho yake huko katika Nchi ya Ahadi naye hakuyapoteza maono yake.

Wenye Kunung'unika Na Kuumwa na Nyoka (Hesabu 21)

Mungu huchukizwa na manung'uniko na kunatanata. Yeye alidhihirisha jinsi ambavyo anavyo chukizwa na kunung'unika wakati alipowatuma nyoka kwao wana wa Israeli walikuwa wakinung'unika naye akawafanya wale nyoka kuwauma wenye kunatanata. Na halafu wakati wengi miongoni mwao walipokuwa wakifa kwa ajili ya kuumwa na nyoka, Mungu alimwambia Musa kumchukua nyoka wa shaba na kumuezeka juu ya mti katikati mwa kambi. Halafu habari njema ikatangazwa kote katika kambi, kwamba ye yote mwenye kuumwa na nyoka aliye nun'unika na aliyekwenda katikati ya kambi na kumtizama yule nyoka wa shaba juu ya mti angeliupata uponyaji.

Wengi miongoni mwao wenye kuumwa na nyoka na wenye kununa wakamtilia shaka Mungu, na kuuliza jinsi ambavyo kukitazama kipande cha shaba kingeliwapa uponyaji kutokana na kuumwa kwa nyoka. Wao wakavimba na kufa. Lakini wengine wakaufanya uamuzi kwamba hata ingawa hapakuwa na maelezo au jambo lo lote la kielimu ya madawa kulihusu jambo hili, kumtumainia Mungu ndiyo tumaini lililokuwa la kipekee walilokuwa nalo. Wao walitambaa na kujikokota, na wengine kubebwa hadi katikati ya kambi na kumtazama yule nyoka wa shaba. Na wao wakaupata uponyaji!

Tunajifunza matumizi ya mfano huu ya ki-Injili wakati Yesu anapotembelewa naye Rabi aliyeitwa, Nikodemu. Wakati huyu Rabi mwenye sifa nyingi huko Yerusalemu alipomwambia Yesu kwamba alikuwa amemtembelea yeye ili kuyasikiliza yale aliyokuwa akiyasema kwa kuwa alikuwa amevutiwa mno na yale alikuwa akiyatenda, Yesu alimkumbusha Nikodemu huu muujiza mkuu katika Agano la Kale. Na halafu Yesu akaulinganisha huu muujiza na yeye mwenyewe. Akamwambia Nikodemu, kama jinsi ambavyo yule nyoka alivyo inuliwa juu ya mti, vivyo hivyo Yesu angeliinuliwa juu ya msalaba. Wote wale wangelimtazama Yeye juu ya msalaba kwa imani, wangeliokolewa kutoka katika shida yao ya dhambi kwa jinsi ile ambayo wale wanunaji walioumwa na nyoka walivyo okolewa kutokana na hatari ya kuumwa na nyoka (Yohana 3:14-16)

Tazama Na Uishi

Je! Umeuchukua mtizamo ule wa imani? Je! Umemtizama Yesu Kristo aliyeinuliwa juu ya msalaba? Je! Umeiweka imani yako na tumaini lako kwa yale yote ambayo Yesu aliyoyafanya hapo kwa ajili yako? Yeye peke yake ndiye suluhisho lako kwa janga la dhambi kwa kuwa Yeye alikuwa ndiye Mwana wa pekee wake Mungu aliyekufa juu ya msalaba kwa ajili yako. Hii yamaanisha Yesu Kristo ndiye mkombozi wa pekee wake Mungu – naye ndiye tumaini lako la kipekee la kupata suluhisho na mwokozi kwa janga lako la umilele la dhambi.

Sura ya Sita

Mwamba na Fimbo (Sura ya 20)

Tunapozidi kuyatazama maisha yake Musa, ni jambo la kututia huzuni kutambua kwamba yeye hakuingia katika Nchi ya ahadi. Mwishowe, Mungu hakumbagua Musa tokana nalo taifa nzima. Dhambi yake Musa ni moja wapo ya siri zilizopo katika kitabu cha Hesabu.

Nakili yatueleza kwamba Bwana alizungumza kwake Musa na kumwambia yeye aichukue fimbo na kulikusanya kundi la watu pamoja. Mungu alimwambia yeye kuuzungumzia ule mwamba nao ungeliyatoa maji kwao watu pamoja na wanyama. Hata ingawa Musa alikuwa nalo shaka, yeye aliwakusanya watu pamoja. Yeye akaupiga ule mwamba mara mbili kwa fimbo yake nayo maji yakatoka katika ule mwamba. Watu pamoja na mifugo yao wakayanywa yale maji. Ndipo Bwana akanena naye Musa pamoja na Haruni, “Kwa kuwa haukuniamini mimi, ili kunitukuza mimi mbele ya macho yao wana wa Israeli, hivyo basi hautangia katika Nchi ya Ahadi.” (Hesabu 20:11-13)

Yapo mambo kadha ambayo tutayatilia maanani tunapoutizama uzito wa adhabu yake Mungu. Jambo la kwanza, sisi tu nani hivi kwamba twaweza kumwambia Mungu kile kilicho cha haki au cha kukubalika. Musa hakulalamika kuhusu adhabu yake.

Kumbu Kumbu La Torati yatueleza sisi kwamba yeye alizungumza naye Mungu hapo siku moja kulihusu jambo hili naye Mungu akasema, “Usizungumze nami zaidi kulihusu jambo hili.” Naye Musa hakulileta jambo hili mbele zake Mungu wakati mwingine ule.

Na la pili, Mungu anayo vipimo au kanuni za juu kwao viongozi kuwaliko watu wa kawaida. Maandiko kwa hakika yatupatia vipimo namna mbili. Unapofanyika mwanachama wa kanisa, zipo kanuni fulani ambazo wahitajika kuishi kwazo. Lakini kanisa, kulingana nayo maandiko, lahitajika kutarajia mengi kutoka kwao viongozi kuliko washiriki wanachama. Mungu hutilia uongozi maanani mno. Musa alikuwepo katika cheo cha uongozi. Dhambi ambayo yawezekana kuonekana duni mno kwao watu wengine haikua dhambi ndogo kwa sababu yake yeye aliyeitenda pamoja na cheo alichowezekwa naye Mungu.

Yaonekana kwa uwazi kwamba dhambi yake ilikuwa ya namna hii. Kwanza kabisa, Mungu alisema, “Zungumza na mwamba ule pale.” Yeye hakuzungumza nao ule mwamba; badala yake yeye aliupiga ule mwamba kwa fimbo yake – mara mbili. Huku kulikuwa ni kutokutii.

Mungu alishitaki Musa kwa dhambi nyingine kubwa. Mungu alikuwa amemfunza Musa kwamba wakati wote yeye alikuwa pamoja naye na kwamba yeye ndiye ambaye angeliwakomboa watu wake, na angelimfanya Musa kuwa ni chombo cha kibinadamu kwa ule muujiza mkuu. Huu muujiza mkuu wa kutoka Misri ulitukia kwa kuwa Musa alikuwa amejifunza kile ambacho Mungu angelikitenda kumpitia mtu ambaye alijifunza kwamba yeye hakuwa ni kitu. Musa alikuwa ameishi kwa miaka arobaini huko jangwani akijifunza siri za kiroho kama vile: "Mimi siye mkombozi, lakini Yeye ndiye, Naye yupo pamoja nami. Siwezi kumkomboa mtu ye yote, lakini Yeye aweza, Naye yupo pamoja nami." Muujiza mkuu ulitendeka kwa sababu Musa angeliyasema yale yaliyotendeka, "Mimi sikuwakomboa hawa watu, bali Yeye alitenda hivyo kwa kuwa Yeye alikuwa pamoja nami."

Musa alipouliza, "Je! Ni lazima Tukuletee wewe maji kutoka kwa mwamba huu?" Yeye hakuwa akimpa Mungu heshima au utukufu na stahi machoni pa watu. Yeye hakuwa akidhihirisha kwa wazi kabisa kwamba ni Mungu ambaye alikuwa akiutenda huu muujiza. Musa alikuwa akiichukua heshima nao utukufu kwa ule muujiza. Hii ilikuwa ndiyo sehemu kuu ya dhambi yake Musa.

Njia ambayo twaweza kuona jambo hili kulingana nao mtizamo wake Mungu ni katika kutambua kwamba Mungu ameweka vipimo au kanuni ambazo yeye mwenyewe ndiye mwenye kuzifahamu. Yeye hushiriki nasi nyingi ya kanuni hizo, lakini kumbuka, ni Mungu ambaye hutufunza sisi kuwa wenye haki, na wala siyo sisi ambao humfunza Yeye. Kulingana na kanuni zake Mungu hukumu ya adhabu yake Musa ilikuwa ni yenye kukubalika na yenye haki. Yaonekana kwamba Mungu alikubaliana naye Mungu. Kuanzia muujiza wa ukombozi kutoka Misri fimbo yake Musa ilikuwa ni mfano wa siri za kiroho ambazo Musa alikuwa amejifunza katika kichaka kilichowaka moto bila ya kuteketea. Na kwa kujifunza kwetu pamoja na matumizi yetu, upo ukweli mkuu kwetu tuwezao kujifunza kutoka kwa dhambi yake Musa wakati alipoupiga mwamba kwa fimbo yake.

"Kuteketea" (Uchovu Kabisa) wake Musa

Katika sura ya kumi na moja ya Kitabu cha Hesabu ipo hadithi nyingine ya muhimu kumhusu Musa. Tunayasikia mengi mno katika siku ya leo kuhusu "Kuteketea", neno ambalo latumiwa nao watu wakati wanapoufikia mwisho wao wenyewe, kimwili, kihisia na kiakili. Hata watu wakuu wake Mungu huupata uchovu, na kwa wakati mwingine wao "huchoshwa kabisa". Ipo tofauti kati ya kuchoka na kuchoshwa kabisa.

Kwa mfano, katika sura hii iliyomo katika kitabu cha Hesabu, twamsikia Musa akimwambia Bwana, "Mimi siwezi kulibeba taifa hili peke yangu. Mzigo huu ni mzito mno. Na kama utanitendea mimi kwa njia hii, tafadhali niue mimi sasa hivi. Itakuwa ni fadhili. Niondoe mimi katika janga hili ambalo haliwezekani." (Hesabu 23:9-11)

Je! Wewe umeshawahi kujisihi hivyo? Na gundua kwamba Musa, Eliya, Ayubu, Daudi, Yohana Mtume, na wengi miongoni mwao watu wakuu wake Mungu katika maandiko walifikia hali hii ya kuchoshwa kabisa hivi kwamba wakamwambia Mungu kwamba wao walitaka kufa mauti. "Kuteketea" hutokea kwao watu wachaji Mungu. maandiko yatueleza kwamba haya yaliwatukia watu wakuu wake Mungu waliopata kuishi kama vile, Musa, Yona, Eliya, Ayubu nao wengine wengi. Lakini wakati hawa watu wake Mungu walipo teketea kwa uchovu mwingi hivi kwamba wakamuoba Mungu kitu kibovu – kwamba Mungu ayachukue maisha yao – Mungu aliwanusuru wao kwa kuwa Mungu aliifahamu mioyo yao.

Tayari Musa alikuwa amefahamu kwamba ni Mungu peke yake ambaye angeliweza kuubeba huu mzigo mkuu wa kuitenda kazi yake ya kimuujiza. Yeye alijifunza jambo lingine lenye umuhimu mkuu kupitia huu ujuzi wa "Kuteketea." Somo hilo lilikuwa kwamba kazi yake Mungu ni jitihada ya timu au kundi la watu. Yeye alitambua hata ingawa Mungu alimtumia yeye, yeye hangeliwahukumu wana wa Israeli akiwa peke yake. Wakati huku kuteketea kwake Musa kulipomleta yeye katika kufahamu hivyo, Mungu alimpa watu sabini ili kumsaidia yeye kuubeba mzigo. Mungu akawapaka mafuta hawa watu sabini kwa Roho Mtakatifu nao wakaongoza chini ya usimamizi wake Musa. Na bila ya kuondoa uongozi kutoka kwake Musa, Mungu aliigawanya kazi katika shehena ziwezao kusimamiwa vyema na vikiwa chini yao watu sabini. Wengi wao wenye kuhitimu kutoka katika vyuo vikuu kwa stashahada ya Masters katika Usimamizi wa biashara watakueleza kwamba hatua tano kwake msimamizi mwenye ufanisi ni: Uchambuzi, Mpangilio, Kupeana Mamlaka, Usimamizi, na halafu Kuugua!

Wakati Musa alipomwendea Mungu akiwa ameteketea kabisa, Mungu alimwambia kwamba roho yake ilihitaji kuhuishwa. Yeye alimwonyesha Musa njia za haki ambazo zingelimpatia yeye pumziko kwa nafsi yake. Njia hizo zilikuwa za kumruhusu Mungu kulitenda lile tu ambalo ni Mungu awezaye kulitenda, na kukumbuka kwamba kazi yake Mungu kupitia watu wake Mungu ni kazi ya juhudi ya timu. Na hivi ndivyo ambavyo Mungu huhuisha watu wake wakati wao ni wenye kuchoshwa kabisa.

Sisi twaishi katika ulimwengu usio na subira nasi twavitaka vitu vyote kwa wakati mmoja. Mungu hatupi sisi vitu vyote kwa wakati mmoja. Kuhuishwa tunakokuona katika maisha yake Musa kulikuwa ni kwa njia iwezekanayo. Badala ya kuirekebisha hali ile mara moja, Mungu alimwonyesha yeye jinsi ya mipangilio na kupeana mamlaka kwao watu wengine ili kusaidia kuubeba mzigo.

Ni jambo la kushangaza kutambua kwamba mtu mkuu kama Musa angeliweza kuteketea kwa uchovu kabisa. Musa aliupata ujuzi huu wa kuteketea kwa uchovu kabisa kwa kuwa yeye ni mwanadamu kila chembe kama ulivyo wewe pamoja nami. Watu wengi hufukiri kwamba wakati unapozaliwa kwa mara yapili na kuwa mwanafunzi wake Yesu, wewe siye mwanadamu wa kawaida tena. Tunapoyatazama maisha yake Musa, tunatambua kwamba hayo siyo kweli. Bibilia imejawa nazo hadithi zao watu wa kawaida ambao walikumbana na kumenyana na kusongwa pamoja na dhiki zile ambazo hutulazimisha sisi kuigundua mipaka yetu ya unyonge wa kibinadamu. Wao ni mifano kwetu kwa kuwa wao waliyatenda mambo makuu wakati Roho Mtakatifu alipouongoza utu wa ubinadamu wao.

Kwa Kutenda au Matumizi

Twaweza kuongeza hadithi yake Musa katika orodha itakayozidi kukua yao watu ambao maisha yao yadhihirisha miujiza ambayo Mungu huifurahia kuitenda mambo yasiyo ya kawaida kuwapitia watu walio wakawaida kwa kuwa wao wapo. Ujuzi ambao Musa aliokuwa nao naye Mungu wadhihirisha kwetu kwamba watu wale ambao Mungu huwatumia ni lazima wajifunze kwamba uwezo mkuu ni kule kuwepo au kujitolea. Uwezo wetu mkuu ni fursa yetu ya kujitolea kwake Mungu. Katika kitabu cha Hesabu twauona ukuu wake Musa, "Kuteketea" kwake Musa, na dhambi yake Musa. Mungu alimtumia Musa kwa kuwa yeye alikuwa yupo. Mungu ataka kututumia mimi nawe kwa kuwa sisi tupo. Je! Wewe umejitolea kwake Mungu? Je! Ungelitaka kujitolea kwake Mungu? Basi, ungana nacho Kilabu makhususi chake na kusema kwake Mungu: "chochote, Popote, na Wakati Wowote. Mimi sijali hii itanifanya mimi kuwa nini. Mimi sijali pale ambapo itanipeleka mimi. Mimi sijali itanigharimu nini. Mimi najitolea!"

Kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati (Sheria)

Sura ya Saba

Wana Wakomaa

Neno hili "Kumbu Kumbu la Torati" lamaanisha "kurudiwa kwa sheria". Lakini Kumbu kumbu la Torati ni zaidi ya kurudiwa kwa sheria. Hiki kitabu cha sheria yenye kuvuviwa na matumizi au utendaji wa sheria yake Mungu kwa kizazi cha pili chao watu wake Mungu.

Kitabu cha Kumbu Kumbu la Torati pia ni nakala ya jumbe kuu ambazo Mungu alizo zihubiri kwa Israeli kabla yao kuvuka Yordani na kuivamia Kanaani. Vifungu vya kufungua vyatusaidia sisi kuelewa kile ambacho Kumbu Kumbu la Torati yazungumzia. Twaelezwa kwamba: "Kitabu hiki cha nakili ujumbe wake Musa kwao watu wa Israeli wakati walipo piga kambi katika bonde la Araba, katika nyika ya Moabu, mashariki mwa mto Yordani. Ujumbe huu ulikuwa umetolewa miaka arobaini baada yao watu kutoka Mlima Horebu." (Kumbu Kumbu La Torati 1:1,3)

Na kama vile tulivyojifunza katika kitabu cha Hesabu, wana wa Israeli walikuwa katika safari jangwani kwa muda wa miaka arobaini. Walikuwa wametoka huko Gosheni, katika Misri, na wao walikuwa wameshuka hadi kwenye Mlima Sinai, hadi huko Kadeshi – Barnea. Na halafu, kwa kuwa wao hawakuwa nayo imani ya kuivamia Kanaani, walikuwa wamezungu-zunguka katika miviringo huko jangwani kwa muda wa miaka thelathini na minane. Kizazi kizima kiliangamia katika jangwa lile!

Mwishowe, wana wa kizazi kile kilicho angamia huko jangwani walikuwa nayo imani ya kuvamia Kanaani. Wao walikuwa wamepiga kambi pande za mashariki wa Mto Yordani kabla ya kupanga kusafiri kupitia Mto Yordani na kuivamia Kanaani. Isipokuwa Yoshua na Kalebu peke yake, kizazi kizima chote kilichokuwa kikiishi wakati wa kutolewa kwa sheria ya kwanza walikuwa wote wame kufa. Kabla ya kuvamia Kanaani, Musa alitaka kuhakikisha kwamba hawa wana walikuwa wamelisikia Neno alilopewa kwa ajili yao na kwa wazazi wao juu ya Mlima Sinai. Na pia alitaka kuwapa changa moto wao ili kujitolea mhanga na kwa dhati katika kuwafunza watoto wao Sheria yake Mungu.

Wakati mwingi waamini wao huranda-randa katika duara nyingi kwa miaka. Wakati wanapoamua kuivamia "Kanaani" yao ya kiroho na kuwa nao ujuzi wa maisha

ndani mwake Kristo ambako Kristo aliwakombolea wao kuwa nayo, wakati wanapochagua wao kupokea kutoka kwa Mungu yale yote aliyonayo kwa ajili yao, wao wako tayari kwa kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati. Kitabu hiki kimejawa nayo masomo kwake yeye ambaye amechagua kuchukua fursa nyingine katika kuyatizama maisha yao mapya katika Kristo na kujitolea kabisa Kwake. Na kama hapa ndipo ulipo, basi kitabu hiki cha Kumbu Kumbu la Torati ni kwa ajili yako.

Somo lingine kuu katika Kitabu hiki cha Kumbu Kumbu La Torati linahusika nalo Neno Lake Mungu katika kufanyika kuwa ni kweli na hakika kwao watu wake Mungu. Katika mojawapo ya jumbe zake kuu, Musa aliwapa changa moto watoto wa kizazi kile kilicho potea kuhakikisha kwamba waliwapitishia na kuwapa wana wao Neno Lake Mungu.

Ujumbe Mkuu wake Musa

Watu wengine hufikiri kwamba Kumbu Kumbu la Torati 6:4-9 ndio ujumbe mkuu ambao Musa aliowahi kuuhubiri. Kifungu hiki cha maandiko chatambulikana kama kuwa ndio itikadi au Ungamo la imani la msingi la Kiyahudi. Hiki ndicho kina cha ujumbe huu:

"Sikilizeni, Enyi Israeli: Bwana Mungu wetu, Bwana ni Mmoja! Utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na nafsi yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya, ambayo ninakuamuru siku ya leo yatakaa ndani ya moyo wako; utawafundisha kwa dhati wanao, utayazungumza unapoketi chini nyumbani mwako, ulalapo, na uamkapo. Utayafunga kama ishara mikononi mwako, na yatakuwa kama utepe katika paji za uso wenu. Utayaandika juu ya vikingi vya milango nyumbani mwenu na katika malango yenu." (Kumbu Kumbu 6:3-10)

Yapo mengi katika ujumbe huu, lakini hiki ndicho kina chake na kina cha Kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati. Kile kwa hakika ambacho Musa alikuwa akikinena kwao hawa watu kabla a kuvuka Mto Yordani na kuivamia Kanaani ni kwamba Mungu aliwaita wao kuwa watu ambao waliompenda kwa utu wao wote. Na ili kwamba waweze kuonyesha upendo wao Kwake, iliwabidi kulitii Neno Lake. Na kwa kulitii Neno Lake, iliwabidi kulifahamu Neno Lake. Mungu aliwataka watoto wao kuwa ni watu ambao siku moja wangelimpenda Yeye kwa utu wao wote. Hivyo basi, Musa aliwahimiza wao kumpenda Mungu kwa utu wao wote, kulifahamu na kulitii Neno Lake, na kuwapa dhamana hizo wana wao.

Misingi Minne ya Uzazi

Yale ambayo Musa alikuwa akiwaambia wao ilikuwa ni jinsi ya kuwafunza wana wao kuwa watu wake Mungu. Mafundisho yanayoelezwa hapa naye Musa yanaegemea juu ya misingi minne. Msingi wa kwanza ni <u>Neno Lake Mungu</u>. Ikiwa watoto watampenda Mungu, basi msingi wa kujifunza kwao ni lazima uwe ni Neno La Mungu. Maandiko yanasema hivi baadaye, "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." (Methali 22:6)

Msingi wa pili ambao mfumo huu wa elimu waegemea ni Wajibu. Ni nani mwenye wajibu kwa malezi ya watoto? Watu wengine hufikiri kwamba wajibu wa elimu ya watoto ni serekali. Wao hutizama shule za jumuia na kufikiri serekali yahitajika kuwafunza watoto yale wanayohitajika kuyafahamu. Wengine husema ni wajibu wa kanisa. Wao huwapeleka watoto wao kanisani kila juma wakifikiri kwamba kanisa litawafunza wao kumpenda Mungu na Neno Lake.

Musa aliuweka wajibu wa Elimu yao watoto juu ya mabega ya wazazi wao. Yeye anawahimiza wazazi - baba kuliruhusu Neno Lake Mungu kudumu katika mioyo yao na halafu kuwafundisha wana wao. Musa amevuviwa na mwenye dhati wakati anapohimiza kwamba baba ndiye ahitajika kuyafanya haya mafunzo ya Maandiko kwao watoto. Maandiko yatazidi katika kutilia mkazo takwa hili.

Msingi wa tatu ambao juu yake mfumo huu wa elimu waelezwa naye Musa waegemea juu ya Uhusiano. Musa alihubiri, "Wakati uamkapo asubuhi pamoja nao, unapoketi nyumbani pamoja nao, unapotembea njiani pamoja nao, na unapolala nyumbani usiku pamoja nao, wafunze Maneno yake Mungu." (Kumbu Kumbu La Torati 6:7)
Wengi wa wazazi akina mababa wao hufikiria hili jambo haliwezekani, kwa kuwa wao hawapo nyumbani wakati watoto wao wanapoamka au kwenda kulala.

Ni bora mno kama utafasiri desturi na mila zako kulingana na mwangaza wa Maandiko kuliko kufasiri Maandiko kwa mwangaza wa desturi yako kibinafsi. Katika hali hii, Bibilia haihitajiki kufasiriwa kulingana na mshururu ulionao kwa ajili ya kazi yako. Mshururu wa kazi yako wahitajika kufasiriwa kulingana nao mwangaza wa haya Maandiko. Ujumbe huu mkuu wake Musa wakuonyesha wewe kuwa nao uhusiano nao watoto wako ambao utawapa umbo lenye nguvu ya desturi ya jamii yako. Hamna jinsi ambavyo waweza kuambatana na maongozi yake Musa na usiwe nao uhusiano nao wanao. Uhusiano ni sehemu muhimu mno katika mfumo wa elimu.

Msingi wa nne ambao juu yake mfumo wake Musa waegemea katika malezi ni ule unaofahamika kama: Kweli. Fanya utambulizi ambao Musa aliousema, "Yaruhusu haya maneno yadumu ndani ya moyo Wako. Wewe mpende Mungu wako kwa moyo wako wote, na halafu yafunze maneno kwa bidii wanao." Usikose ukweli huu wa muhimu. Watoto wetu hujifunza mengi kwa yale tunayoyatenda na jinsi tulivyo kuliko yale tunayoyasema.

Yesu akasema, "Nionyeshe mimi hazina yako, na utanionyesha mimi dhamana zako ni zipi. Nionyeshe mimi dhamana zako, nawe utanionyesha mimi pale ambapo moyo wako ulipo." (Mathayo 6:20-22) Na kwa lugha sanifu, maana yake ni, Nionyeshe mimi pale na jinsi ambavyo unavyotumia mali yako, na jinsi ambavyo unavyoutumia wakati na nguvu zako, nawe utanionyesha mimi pale ambapo moyo wako upo. Watoto wetu hujifunza mengi mno katika kututizama jinsi ambavyo sisi tunavyoishi kuliko jinsi wanavyosikiliza yale tunayowafunza kuhusu dhamani zetu. Yale tunayoyafunza watoto wetu siyo yale tunayowasomea kuhusu dhamana, ila yale yaliyo ya dhamana kwetu sisi.

Misingi minne ambayo ramani kuu yake Musa yaegemea kuhusu malezi ya watoto ipo juu ya Neno Lake Mungu, Wajibu, Uhusiano na kweli.

Sura ya Nane

Kumbu Kumbu Za Miujiza

Kote katika Kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati upo mkazo juu ya umuhimu katika kulitii Neno La Mungu. Wakati Israeli walipozitii sheria zake Mungu, Yeye aliwabariki wao. Wakati ambapo wao hawakuzitii sheria zake Mungu, wao hawakuzifurahia baraka zake Mungu. Musa anayaonyesha haya yote kwa ufasaha mkuu na halafu anahubiri kwamba ni lazima walitii Neno Lake Mungu. Neno mmoja wapo lenye umuhimu mkuu katika kitabu hiki, ni "Kutii".

Sababu kuu yake Musa katika ujumbe wake wa kwanza katika Kumbu Kumbu La Torati ilikuwa kuwasaidia hawa Waebrania kukumbuka jinsi ambavyo Mungu alivyofanya kazi katika maisha ya wazazi wao na kukumbuka miujiza ambayo Mungu aliwatendea wao. Musa alitumainia miujiza ambayo Mungu alikuwa amewatendea katika msafara wao huko jangwani kwa wazazi wao ungelikuwa na uzito wenye maana na matokeo katika maisha ya kizazi hiki, na kwamba wangeliwaeleza watoto wao kuhusu miujiza hiyo.

Musa pia alihubiri akitilia mkazo mkubwa kwamba yawabidi kwamba wasije wakalivunja Agano lao naye Mungu. Agano ni kandarasi kati yake Mungu nao watu Wake. Matakwa ya kandarasi ile hua yamenakiliwa. Na kama watu hawataambatana na matakwa ya kandarasi ile, hamna kandarasi. Mungu hawajibiki kuwabariki wao kama wao si watiifu.

Sura ya tano ni marudio ya Amri Kumi. Linganisha maneno ya amri zilizopo katika Kitabu cha Kutoka (Sura 20) na marudio ya maneno yaliyomo katika Kumbu Kumbu La Torati. Kama ukinlinganisha kwa makini nakala hizi mbili za Amri Kumi, utaupata mwangaza mpya katika hizi sheria zake Mungu. Katika kurudia huku kwa hizi Amri, Musa anawaambia Waebrania wawe na mioyo kwa Mungu na kuzitii Amri zake. Na kama wakitenda hivyo, yote yatakuwa mema kwao katika siku zao za usoni na pamoja na watoto wao katika vizazi vyao vyote.

Katika kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati Musa aliwahubiria watu kwamba: "Ni lazima mzitii amri zote zake Bwana Mungu wenu, mkiyafuata maongozi yake yote katika kila maelezo , na kuenenda katika njia yote ambayo ameiweka mbele yenu. Hapo ndipo mtapata kuishi maisha marefu na yenye mafanikio." (Kumbu Kumbu La Torati 27:9-11)

Ujumbe mkuu wake Musa katika sura ya sita, ambao umefanyika kuwa ni Ungamo la msingi la imani, waitwa "Shema", (Maana yake "Sikia" katika Kiebrania), kwa sababu huu ujumbe waanza kwa kusema, "Sikilizeni, Enyi Israeli." Sababu ya ujumbe huu ilikuwa ni kuwapa changa moto kizazi cha pili cha watu wake Mungu ili kuwapitilizia wana wao Neno la Mungu, kizazi cha tatu cha taifa la Israeli. Twaipata ramani yake Musa kwao wazazi kuhusu ulezi wa watoto katika ujumbe huu wa kuvutia wake Musa.

Sura ya nane ya Kumbu Kumbu La Torati yatupatia ujumbe mwingine wenye ufasaha na uzito wake Musa. Huu ni ujumbe kuhusu umuhimu wa kulitii Neno La Mungu. Musa pia atuonyesha hapa jinsi tuwezavyo kujifunza Neno Lake Mungu. Ujumbe huu mkuu watueleza sababu ya Neno Lake Mungu. Mungu alitupatia Neno Lake kwa sababu yeye atutaka sisi kufahamu jinsi ya kuishi. Mungu alituumba sisi naye afahamu jinsi ambavyo twaweza kuwa na maisha yenye kutosheleka. Yesu alikuja akisema hivi, "Nimekuja ili wawe na uzima kisha wawe nao tele." (Yohana 10:10) Musa atuambia hivi katika ujumbe huu wake mkuu jinsi ambavyo twaweza kuingia katika huu uzima tele. (Kumbu Kumbu La Torati 8:1-14)

Musa anahubiri kwamba Neno lake Mungu ni kuhusu Uzima. Na kama wataka kulielewa Neno Lake Mungu, zipo yamkini njia mbili uwezavyo kujifunza. Waweza kujiunga na vyuo vikuu, Seminari, au shule ya Bibilia. Na pia waweza kulisoma Neno Lake Mungu kwa kiakili au kwa kielimu ukiwa mwenyewe. Lakini kulingana naye Musa, hiyo siyo njia ya pekee kujifunza Neno lake Mungu. Ikiwa Neno lake Mungu ni kuhusu maisha, hivyo basi njia nyingine ya kujifunza Neno lake Mungu ni kwa kupitia kujifunza

kuhusu maisha. Neno hutupa mwangaza kuhusu maisha nayo maisha hutupa mwangaza kulihusu Neno La Mungu.

Wakati Mungu anapoturuhusu sisi kukaa njaa na kupitia katika dhoruba ya dhiki za maisha, sisi humgeukia Yeye na kutambua kwamba Yeye ndiye kina cha maisha na kile chote tunachokihitaji kwa kuyaishi maisha jinsi ambavyo alivyoyafuma maisha na kuyataka yawe wakati alipotuumba sisi. Ni kwa kuranda-randa jangwani kwetu, na kwa kupitia ujuzi wetu mugumu katika maisha, ambako Mungu hutufanya sisi kufahamu kwamba "Mwandamu hataishi kwa mkate peke yake." Mwanadamu huishi kwa kulitii kila Neno ambalo Mungu amempatia yeye. Wana wa Israeli hawakujifunza Neno lake Mungu katika Seminari au katika Sinagogi. Wao walijifunza Neno lake Mungu katika mazingara ya hali yao ya ujuzi wa kweli wa kimaisha.

Somo lingine ambalo twajifunza kutoka katika sura ya nane ya Kumbu Kumbu La Torati ni kujikinga dhidi ya hatari za mafanikio. Je! Wafahamu kwamba baraka zitokanazo kwa fanaka zaweza kuwa ni changa moto? Hawa watu waliochaguliwa walikuwa wamejifunza Neno lake Mungu kwa kupitia dhiki na nidhamu yake Mungu. wakati walipoadhibiwa kwa kutokutii kwao, wao walijifunza kwamba Neno lake Mungu lilikuwa ndio ufunguo kwa maisha.

Musa sasa anawaonya wao kwamba ni lazima wayatende yale waliyojifunza katika nyakati ngumu katika maisha yao wakati Mungu anapowapa baraka tele wao: "Msije mkasahau masomo yale mliyojifunza katika dhiki yenu na katika nyakati za majaribu. Unapofikia mahala pale ambapo unafanikiwa, huo ndio wakati wa kujihadhari." Nakala ya Agano Jipya ya ujumbe huu ni, "Hebu yeye ajidhaniaye kwamba amesimama, ajihadhari asije akaanguka." (1 Wakorintho 10:12)

Musa anafuatilia ujumbe huu mkuu kuhusu Neno lake Mungu na ujumbe mwingine mkuu kuhusu neema yake Mungu. Marudio kwa ajili ya kutilia mkazo, yeye awaambia hawa watu kwa mara nne kwamba wao hawakuchaguliwa naye Mungu kwa kuwa wao ni wema na hivyo basi wastahili rehema yake Mungu: "Yehova Mungu wako hakupi hii nchi kwa kuwa wewe ni mwema, ni kwa sababu wewe si mwema. Wewe ni mwovu, na watu wenye shingo ngumu." (Kumbu Kumbu La Torati 9:4-6)

Hii ni picha ya kuvutia mno kuhusu neema yake Mungu. Rehema zake Mungu hutulinda sisi kutokana na adhabu tupasayo kuipokea. Neema yake Mungu na wingi wake hutupa rehema na baraka zake Mungu ambazo sisi hatustahili. Mungu hatubariki sisi kwa kuwa sisi tu wema. Mungu hutubariki sisi kwa kuwa Yeye ni mwema na yeye atupenda sisi. Hii ndio maana yake neno hili "Neema".

Musa atupa sisi maelezo yaliyo wazi kabisa kuhusu neema yake Mungu katika ujumbe huu mkuu uliopo katika sura ya tisa katika Kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati. Utaona mkazo kuhusu neema kote katika Bibilia kwa kuwa Neema yake Mungu ni yenye tabia yake Mungu yenye uwezo tunayoipata katika kiini chetu cha wokovu. Neema yake Mungu haipatikani kwa kuifanyia kazi au kuwa nayo tabia njema kutoka kwetu sisi.

Sura ya Tisa

Jumbe Kuu Zaidi Zake Musa

Kwa kuwa tumetilia maanani ujumbe mkuu wake Musa kuhusu neema yake Mungu katika sura ya tisa, tupo tayari kutafakari ujumbe wake kuhusu kuitika kwetu kwa Neema yake Mungu katika sura ya kumi.

"Na sasa, Israeli, ni jambo gani ambalo Bwana Mungu wenu alitaka kutoka kwenu, isipokuwa kumcha Bwana Mungu wenu, kutembea katika njia Zake zote na kumpenda

Yeye, kumtumikia Bwana Mungu wako kwa roho yako yote na kwa nafsi yako yote, na kuziweka amri zake Bwana na sheria ambazo nakuamuru siku yaleo kwa uheri wako? Hakika mbingu na mbingu zilizo juu ni mali yake Bwana Mungu wako, pamoja nayo nchi na yote yaliyomo ndani mwake. Mungu alipendezwa nao babu zenu, ili kuwapenda wao; naye akawachagua wajukuu zao baada yao, nyinyi miongoni mwa watu wote, kama ilivyo siku ya leo. Hivyo basi itahirisheni mioyo yenu, na msiwe wenye shingo ngumu tena."

Mkazo uliopo mahala hapa ni jinsi ambayo sisi twaipokea neema yake Mungu. Mungu hutupenda sisi hata nyakati ambazo tunazo shindwa. Hamna cho chote kile tunachokifanya kiwezacho kutufanya sisi kuupokea upendo wake, kwa kuwa upendo Wake haupatikani au kupotezwa kulingana na juhudi yetu.

Hamna chochote kile uwezacho kukitenda cha weza kumufanya Mungu aache kukupenda wewe. Upendo wake hautegemei cho chote kile. Upendo wake Mungu ambao hautegemei cho chote kile hutia nguvu rehema na neema zake Mungu. Hii ndiyo maana yake "Neema". Neema ni upanga ukatao kuwili. Huo hukata kuwili. Kwanza, hiyo husema maneno kwamba upendo wake Mungu pamoja na baraka Yake hazitegemei juhudi nyingi uliyo nayo. Unapoyaelewa maneno ya neema, rehema na upendo kama yanavyo dhihirisha tabia na utu wake Mungu, utafahamu kwamba hautakikani kuwa nayo hofu kuhusu kujaribu kuupokea upendo wake Mungu. Yeye ataedelea kukupenda wewe kwa vyo vyote vile, kwa sababu ya kiini cha rehema, neema, na upendo Wake.

Hauwezi kupoteza rehema, neema au upendo wake Mungu kwa sababu ya juhudi iliyo kinyume. Mungu hakupendi wewe kwa kuwa wewe umwema naye hataacha kukupenda wewe ikiwa utakuwa mwovu. Mungu akupenda wewe. Yesu akupenda wewe wakati wewe ni mwovu, hata ingawa hii humfanya yeye kuwa na huzuni mno. Lakini, Yesu akupenda wewe. Huu ndio ujumbe uliomo katika Bibilia nzima, na huu ndio ujumbe wa Kumbu Kumbu la Torati.

Je! Waweza kupokea rehema, neema, na upendo wake Mungu? Njia nyingine ya kuliuliza swala hilo hilo ni katika kukuuliza wewe, "Je! Wampenda Mungu kwa kiasi kigani?" Mwanamke mmoja mchaji Mungu aliyepata kuishi katika karne nyingine alisema hivi, "Afadhali niende jehanamu kuliko kumkasirisha Roho Mtakatifu kwa mara nyingine moja." Twahitajika kutaka kumpendeza Mungu huyu, ambaye atupenda sisi kwa vyo vyote vile, na hatutakikani kutaka kumjeruhi Mungu huyu kwa kuwa twampenda Yeye. Hili latutia moyo sisi kuyasafisha maisha yetu kutokana nayo mambo ambayo hayampendezi Yeye na halafu, tumtumikie Yeye na kudhihirisha upendo wetu katika kumpenda na kumuabudu kwa shukurani.

Baada ya kutueleza mengi kuhusu neema yake Mungu pamoja nao wokovu wetu, mtume Paulo ayasema haya kwetu sisi, "Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure." (2 Wakorintho 6:1). Kama ilivyo dhambi kulitaja jina la Mungu bure, pia ni dhambi kuipokea neema yake bure. Ikiwa Mungu atupenda sisi na kutupatia kwa wingi baraka zake kwetu sisi kwa neema, ikiwa hatutatenda cho chote na hiyo neema, sisi twatenda dhambi ya kulichukuwa jina la Bwana bure. Ujumbe mkuu wake Musa katika sura ya kumi watuonya sisi tusije tukaipokea neema ya Mungu Bure.

Hii yafuatiwa na ujumbe kuhusu uasi (sura ya 13). Uasi wamaanisha, "kusimama au kuanguka mbali kutoka katika msimamo ambao umeuchukuwa naye Mungu." Musa aliwaambia hawa watu, kwamba ikiwa mwana, au binti, au mke pamoja na rafiki wa karibu akijaribu kuwavuta mbali na Mungu, wahitajika kumuagamiza yule mtu bila ya kuwa na huruma juu yake. Akawaambia kwamba wakiufikia mji wenye kuasi, wahitaji kuuharibu ule mji. Hili laonekana kuwa ni jambo lenye ukali mkuu, lakini kama ukiyachunguza matokeo ya uasi – Mateka ya Babuloni, Mateka ya Ashuri – utaona sababu yake Mungu kuwa mkali wakati alipomwonyesha Musa jinsi ya kukumbana na shida ya uasi.

Musa pia alihubiri ujumbe kuhusu Fungu la Kumi (14:22-28). Neno hili “Fungu la Kumi” katika Kiebrania lamaanisha “Moja kwa Kumi”. Tumeamrishwa kumtolea Mungu moja kwa kumi kwa yale yote tuliyonayo. Kutoa fungu la kumi kwa tufundisha kumweka Mungu mbele katika maisha yetu. Mungu hahitaji fungu la kumi kutoka kwa mapato yetu. Mungu aliitoa amri ya fungu la kumi kwa sababu ni njia moja wapo tuwezayo kupima kujitolea kwetu Kwake. Kweli ya muhimu ambayo Mungu atufundisha kupitia kutoa kwa fungu la kumi twajifunza wakati tunapoelewa kwamba fungu la kumi ilikuwa sehemu ya kwanza ya kumi kutoka kwa yale yote ambayo watu waliochaguliwa waliyapata mapato yake au kupokea kutoka kwake Mungu alipokuwa akikutana nayo mahitaji yao. Mungu afahamu kama yeye ndiye wa kwanza ama sivyo katika maisha yetu, hata ingawa wakati mwingine sisi hatufahamu. Hii ndiyo sababu Mungu ametuwamuru sisi kuonyesha kwamba Yeye ndiye wa kwanza katika dhamana zetu kwa kumtolea Mungu sehemu ya kwanza ya kumi katika yale yote tunayoyapokea.

Mungu ataka sehemu ya kwanza ya kumi. Wakati Waebrania walipoingia katika nchi ya Kanaani, mji wa kwanza waliouteka ulikuwa ni Yeriko. Yale yote yaliyotekwa nyara katika mji ule yalimwendea Mungu kwa kuwa ulikuwa ndiyo mji wa kwanza kutekwa.

Yapo maneno mawili ambayo yanaeleza maana sahihi kuhusu vitabu, sura, na vifungu katika Bibilia. Maneno hayo mawili ni haya: MUNGU KWANZA! Kumweka Mungu kwanza silo jambo rahisi, lakini kumweka Mungu kwanza silo jambo lenye kutatanisha. Sisi hukitatanisha kile kinachomaanisha kumweka Mungu kwanza kwa kuwa hatutaki kumweka Mungu kwanza. Fungu la kumi hutusaidia sisi kuwa wa kweli sisi wenyewe na kukipima kiwango ambacho Mungu ni wa kwanza katika maisha yetu.

Katika sura ya kumi na tano kwenye kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati, Musa atupa sisi ujumbe mkuu kuhusu umuhimu wa ukarimu wetu kwao walio maskini. Sheria yake Musa yatilia mkazo mkubwa kuhusu ukarimu na kote katika Agano la Kale. Musa anapeana njia kadha za mwongozo kuhusu jinsi ambavyo fungu la kumi lao watu wake Mungu lahitajika kugawanywa. Yahitajika kutolewa kwao Walawi – Huu ndio msingi wa kuwalipa wafanya huduma kanisani katika Bibilia. Yahitajika kutolewa kwake mgeni katika nchi ile na ambaye ni mwenye kuadhirika. Wana wa Israeli pia walishurutishwa kuwapa wajane pamoja na watoto yatima miongoni mwao.

Wakati Musa aliponena nao watu kuhusu ukarimu, yeye alisema, “Nyinyi ni watu wenye shingo ngumu.” Aliwaonya wao wasije wakanung’unika kuhusu kushiriki nao wale wenye mahitaji (15:1-11). Yeye ahubiri kwamba wakati wote kutekuwepo nao watu maskini miongoni mwao na ndio sababu amri hii ilikuwa ni ya muhimu.

Na kama nabii, Musa aliwaambia Neno la Mungu kama muhubiri mkuu. Na pia aliwaeleza mambo yajayo wakati alipolihubiri Neno La Mungu. Israeli hawakuwa naye Mfalme na wao hawangelimpata kwa miaka mingine mia tano. Tutasoma maelezo sahihi kuhusu jinsi walivyo mvisha taji mfalme wao wa kwanza tutakapokifikilia kitabu cha Samweli wa kwanza. Lakini Musa alikuwa amewaambia wana wa Israeli kwamba siku mmoja Mungu atakutana nayo matarajio yao na kuwapa wao mfalme. Halafu yeye kwa njia ya kiunabii akaandika amri katika vitabu vya sheria vyenye uvuvio kwamba wakati watakapowapata wafalme wao, mfalme wao ni lazima anakili sheria kutoka kwa nakala ya kitabu kilichowekwa nao makuhani wa kilawi na kukisoma kila siku ya maisha yake ili akajifunze kumheshimu Bwana na kutii sheria Zake. Huku kulisoma neno lake Bwana kwa kila wakati kungelimzuia yeye kujidhania kwamba yeye ni bora kuwaliko wale wengine. Na pia kungelimzuia yeye kuigeukia mbali Sheria ya Mungu, na ingalimpa yeye, utawala mrefu na bora.

Zaburi yake Daudi ya Kwanza, yeye ataja tabia yake mtu aliye barikiwa au mwenye heri kama mtu ambaye hutafakari Sheria yake Mungu usiku na mchana. Yeye pia huzitaja baraka alizonazo mtu huyu kwa kuwa yeye hulifurahia Neno Lake Mungu na kutembea katika mashauri anayoyapata katika Neno lake Mungu. Na kwa kuwa Daudi alikuwa ndiye mfalme wa pili wa Israeli, ilimbidi kutii amri hizi za kiunabii zake Musa. Baraka zake mtu aliyebarikiwa ambazo Daudi anazionyesha katika Zaburi ya kwanza ni kama hadithi yake Daudi ya maisha yake ya kiroho. Sababu ambazo Musa aziamuru hizi sheria zilitimilika katika maisha yake Daudi.

Katika sura ya Kumi na nane ya Kumbu Kumbu la Torati, upo ujumbe mkali kuhusu mambo ya ushirikina. Musa anatumia lugha nzito mno ili kueleza wazi kwamba Mungu hapendelei mambo kama kupiga ramli au wenye kuzungumza na wafu. Ujumbe huo wasema hivi:

"Hamna Mu Israeli ambaye akubaliwa kushiriki katika mambo ya uchawi au kuwaita roho wachafu kwa usaidizi au kupiga ramli au kuwachezea filimbi nyoka, ushirikina au uchawi, au kuziita roho zao watu waliokufa. Ye yote atakayeyatenda mambo haya yeye ni chombo cha kutishia na kuchukiza kwake Mungu. Na ni kwa sababu tabia hizi ndiyo maana yake Bwana Mungu wenu atawahamisha wao.

Mataifa ambayo mtayachukuwa makao yao wameyatenda haya mambo yote, lakini Bwana Mungu wenu hatawaruhusu nyinyi kuyatenda haya mambo." (18:9-14)

mwungwana mmoja amenena kwamba yapo mambo mengi kati ya mbingu na dunia ambayo mwanadamu hajawahi hata kuyaota. Ni vyema kama ukitambua kwamba maandiko hayajayasema kwamba hayapo. Yatueleza sisi tujitenge mbali kutoka kwayo. Zipo roho katika ulimwengu wa roho ambazo siyo takatifu na wala siyo zake Mungu. Unapohusika na mambo ya ushirikina, na yale yote yanayohusika nayo, wewe wahusika na roho ambayo siyo yake Mungu. Mungu kwa kumpitia Musa, hivyo basi awakanya watu wake kutokuhusika na roho za ulimwengu wa gizani ambao hauhusikani naye Mungu. Wazo lake Mungu kupitia kwake Musa yaonekana kwamba tunaye Roho Mtakatifu wake Mungu kutuongoza kwenye roho za ulimwengu wa kimbiguni. Hivyo basi ni dhambi kwetu sisi kuhusika nao ulimwengu wa roho chafu kuyapata maongozi, mwongozo au kupata kupokea nguvu katika njia ye yote yale.

Upo ujumbe mkuu katika kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati kuhusu Masihi nabii. Musa alisema, "Siku mmoja nabii atakuja ulimwenguni. Mlipokuwa katika Mlima wa Sinai na Mungu kutoa sheria, nyinyi mlimwambia Yeye, kunipitia mimi, 'Ee, hatumtaki Mungu kuzungumza nasi. Hatuwezi kusimama kuisikiliza sauti yake Mungu.'" (Kumbu Kumbu La Torati 18:15-17) Musa aliliambia taifa la Israeli kwamba Mungu aliyasikia maombi yao na angalimtuma nabii katika ulimwengu ambaye angelinena kumpitia yeye.

Mungu aliwapa maneno yalioandikwa kwa njia ya muujiza, lakini alitaka kuzungumza nao kwa njia ya zaidi ya maneno yalioandikwa. Katika rehema na upendo wake kwao, Mungu alikuwa atawazungumzia wao kumpitia nabii makhususi. Nabii huyo alikuwa ndiye Masihi ambaye angelikuwa nabii, kuhani na mfalme.

Zipo jumbe kuu katika sura ya kumi na tisa kuhusu adhabu kuu. Mkazo haupo juu yake mtuhumiwa na aibu iliyopo katika kifo chake mtu. Maneno yenye uvuvio yake Musa kuhusu adhabu kuu, ni yao wenye kuadhiriwa naye yule mtuhumiwa. Andiko hili latuambia sisi kwamba adhabu kuu itausafisha uovu katika Israeli.

Ujumbe mkuu kuhusu imani wapatikana katika sura ya ishirini. Gidioni atautumia ujumbe huu wakati atakapoliongoza jeshi kinyume cha Wamidiani ambao walikuwa wamewateka Israeli (Waamuzi 7:1-7).

"Unapopigana na jeshi lililo kuu kukuliko wewe, kumbuka, tumaini lako ni kwamba Mungu yupo pamoja nawe. Imani ndiyo yatakikana kuwa nayo wakati unapowavamia majeshi yaliyo makuu kuliko wewe." (Kumbu Kumbu La Torati 20:6-8)

Twaiona dhana ya "Neema" ikidhihirishwa mara nyingi katika kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati. Pia twakumbana na dhana kuhusu "Wokovu". Sheria ya kuhusu mkombozi wa kijamii katika Kumbu Kumbu La Torati 25 ni picha yenye kuvutia yake Mwokozi, Yesu Kristo. Mara ya kwanza unapokutana nalo neno "Mkombozi" au "Ukombozi," haya maneno ni ya kisheria. Lakini kama waelewa maana ya kisheria kuhusu ukombozi, waweza kufahamu ukombozi wakati Agano La Kale na Agano Jipya latumia dhana hii kwenye kifo chake Yesu Kristo msalabani. Kifungu hichi katika sura ya ishirini na tano, kinachotupa sisi sheria yake mkombozi wa kijamii, ni ufunguo ambao wafungua maana na matumizi ya kitabu cha Ruthu.

Hapo mwishoni katika kitabu cha Kumbu Kumbu La Torati, Walawi, na Yoshua, utapata amri kuu kutii Neno Lake Mungu. Hili kwa mara nyingine ndilo jambo kuu katika Kumbu Kumbu La Torati. Baadhi ya mahubiri makuu ambayo yamewahi kusikika yapo katika sura za mwisho katika Kumbu Kumbu La Torati, pale ambapo Musa aliahidi baraka yake Mungu juu yao watu Waebrania kama ikiwa wao watalitii Neno lake Mungu au upinzani wake Mungu kama wasipotenda hivyo. Musa aliyamalizia haya mahubiri yenye nguvu kwa kunena: "Nimeweka mbele yenu uzima na mauti. Ee, kama mngelichagua uzima; ili nyinyi pamoja watoto wenu mpate kuishi!" (Kumbu Kumbu La Torati 30:19)

Kitabu Cha Yoshua

Sura ya Kumi

Miliki Milki Yako

Kitabu cha Yoshua kwa njia nyingine ni kinyume cha Kitabu cha Hesabu. Hesabu ni hadithi ya kutoamini ambako watu Waebrania waliangamia kutokana na kutokua kwa imani kwao. Kitabu cha Yoshua ni kuhusu imani, namna ya imani yenye ushindi na humiliki yale yote ambayo ni mapenzi yake Mungu kwa ajili ya watu Wake.

Tulipokikagua kitabu cha Kutoka tulijifunza kwamba jina hili, "Kutoka" maana yake "njia ya kutoka nje"kwenye utumwa mbovu wa Misri. Hiki kitabu cha kwanza cha historia chaweza kuitwa, "Kuingia ndani" katika Nchi ya Ahadi ya Kanaani. Hoja kuu katika kitabu cha Yoshua ni, "Miliki Milki yako."

Jina hili Yoshua ni sawa na lile jina Yesu. Yesu ndivyo linavyotamkwa katika Kiyunani (Griki). Yoshua, au Ya-shu-a, ndivyo ambavyo latamkwa nao Waebrania. Jina hili lamaanisha "Mwokozi" or "Yehova Mwokozi". Katika jina lake, huyu kiongozi mkuu ni picha yake Kristo kwa kuwa Yeye huwaongoza watu wake katika Nchi ya Ahadi ya baraka za kiroho.

Neno lenye Ufunguo katika wokovu kutoka katika Misri yetu ya kiroho ni neno, "Kuamini". Neno lenye ufunguo katika kuingia katika Nchi Ya Ahadi ya Baraka za kiroho zake Mungu ni Neno, "Kutii". Twazungumzia kuhusu imani wakati tunazungumzia kuhusu Kutii. Neno imani lamaanisha kujitolea, kujitolea ambako kunautiifu.

Yoshua alikuwa na umri wa miaka arobaini wakati wa Kutoka Misri. Kumbuka kwamba Yoshua na Kalebu walikuwa ndiyo manusra wawili kutoka huko jangwani kwa sababu wao walileta habari njema walipokuwa wametumwa huko Kanaani kama wapelelezi. Mungu aliiona imani yao kama kitu kinacho stahili dhawabu kuu. Yoshua

alikuwa mwenye umri wa miaka themanini alipopokea amri kuwaongoza watu katika Nchi ya Kanaani na kuvamia mataifa sabini ambayo yalikuwa yakiikinga nchi ile. Yeye hakuipokea amri yake moja kwa moja toka kwake Mungu, ila kutoka kwake Musa, mtu wa Mungu ambaye alimfahamu Mungu na ambaye alimfahamu Yoshua.

Uhusiano katika yake Musa na Yoshua ni mfano mkuu kama ule wa uhusiano wake Paulo/Timotheo na ambao ni wa muhimu mno katika kuwatayarisha viongozi kwao watu na kwa kazi yake Mungu (II Timotheo 2:2). Yoshua alikuwa mwenye umri wa miaka mia moja na kumi wakati alipofariki. Yeye alikuwa ni mtu mwenye uwezo, utiifu, na imani kuu.

Tunapomtizama Mungu akitenda kazi kupitia kiongozi Nabii/kuhani, tunaona mabadiliko ambayo ni muhimu tunapokuja katika uongozi wake Yoshua. Musa alipokea Neno lake Mungu juu ya Mlima Sinai moja kwa moja kutoka kwake Mungu, kama jinsi ambavyo alipokea amri zake katika kichaka kilichokuwa kikiteketea moja kwa moja toka kwake Mungu. Lakini sasa twasoma kwamba Yoshua aelezwa kulitafakari Neno Lililoandikwa –Neno ambalo lilikuwa tayari limetolewa na Mungu kwake Musa. Kama wafalme wa Israeli ambao walikuwa wafuatane naye, Yoshua ameamriwa kufikiria kuhusu Neno Lake Mungu, mchana na usiku, na kwamba ni lazima azitii hizi amri zake Mungu.

Kama vile ambavyo Waebrania walikaribia kuvuka mto wa Yordani na kuivamia Kanaani, haya ndiyo yale ambayo waliambiwa, “Kila mahala ambapo Nyayo za miguu yenu zitakanyanga juu yake, hapo nimewapa nyinyi, kama vile nilivyo sema kwake Musa.” (Yoshua 1:3) Walikuwa wamepewa Nchi nzima, na kwa jinsi ya kufanyika mali yao ilikuwa ni yote, lakini siyo katika kufanyika milki. Sheria ya kumiliki ilikuwa ni kwamba kila mita miraba ya Nchi ya Kanaani ambapo miguu yako itankanyanga juu yake, hiyo ndiyo nitakayokupatia wewe – bila ya kupungukiwa wala kuongoezeka.

Hivi ndiyvo ilivyo katika baraka zetu za kiroho. Zipo baraka nyingi mno za kiroho ambazo zipo kwa ajili yetu siku ya leo: Maombi, Maandiko yenyewe, ushirika, kuabudu – Mungu hutujalia haya yote kwake kila mwamini. Lakini baadhi ya waamini wao huzimiliki baraka hizo hali wengine hawapati kuzimiliki. Ufunguo huu watendeka. Ni lazima ukanyange kwa Nyayo zako juu yake. Wewe humiliki maombi kwa kuomba, wewe humiliki ibada kwa kuabudu, na kuyamiliki Maandiko unapo yasoma, na kuyaelewa, na kuyatenda yasemavyo. Wewe waimiliki Milki yako ya kiroho nyayo moja, unyayo mmoja kwa wakati mmoja.

Wasomi wengi husema kwamba Kitabu cha Waefeso ndicho katika Agano Jipya Kile ambacho Kitabu cha Yoshua kilivyo katika Agano la Kale. Kitabu cha Waefeso cha tuambia sisi kuhusu yale yote kuhusu baraka za kiroho tulizo nazo katika Kristo na kwamba yawezekana kwetu sisi kuingia katika Kristo na kumiliki baraka zote za kiroho.

Msitari wenye ufunguo katika Kitabu cha Yoshua ni Yoshua 1:3. Msitari wenye Ufunguo katika Kitabu cha Waefeso ni Waefeso 1:3, ambao wanena kama jinsi ambavyo msitari wenye ufunguo wa Yoshua: “Abarikiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ametubariki sisi na baraka zote za kiroho katika ulimwengu wa kiroho katika Kristo.” Mungu ametupatia sisi cheti cha baraka zote za kiroho ambazo ametupatia sisi, lakini ni lazima tupafikie pale zilipo na kuzimiliki hizo.

Katika Kitabu cha Yoshua baraka hizo zipo katika Nchi ya Ahadi. Katika Kitabu cha Waefeso zipo katika Kristo. Kama twataka kumiliki hizi baraka za kiroho, lazima tuzipate katika kuwa ndani yake Kristo. Ni lazima tusongelee mahala pa kimbinguni kwa kuwa hapo ndipo zote zilipo. Kitabu cha Joshua chatufundisha kwamba twaweza kuingia katika “Nchi ya Ahadi” ya baraka zake Mungu kwa imani. Paulo atuambia sisi yale yale wakati anapoandika waraka wake wenye kuvuviwa kwao Waefeso.

Waandishi wengine wa Agano Jipya wameandika kuhusu “Nchi ya Ahadi” ya kiroho. Hebu sikiliza mtizamo wake Petro kuhusu wapi na jinsi ya kumiliki milki zetu za

kiroho: "Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe." (II Petro 1:3)

Petro hangeliweza kuandika wala kusoma (II Petro 5:12; Matendo 4:13). Mkazo wake ulikuwa katika kumjua Mungu. Petro hakuwa ni msomi, lakini alikuwa ni jitu la kiroho; yeye alimjua Mungu. Yeye atuambia sisi kwamba Mungu ndiye kina cha baraka zote za kiroho ambazo Mungu ametupatia sisi ushirikiano naye Mungu (II Petro 1:3). Kulingana na Petro, tayari Mungu ametupatia sisi yale yote tunayoyahitaji ili kuishi maisha ya utauwa. Lakini, kumiliki milki yetu ya kiroho, ni lazima kuzidai katika ushirikiano wa ujuzi ufahamu wake Mungu.

Viongozi wawili wakuu wa Kanisa la Agano Jipya wakubaliana wao kwa wao pamoja na Yoshua kwamba twashikilia cheti kinachosema kwamba twamiliki kila baraka tunayo ihitaji. Lakini ni lazima tuzimiliki hizo baraka, hatua mmoja kwa wakati mmoja, katika uhusiano wetu na Mungu, pamoja na Kristo.

Yoshua asema sisi tunayo mambo yote, Petro asema kwamba tunayo yote, Paulo asema kwamba tunayo yote. Ni kwa sababu gani sisi kwa hakika hatuyamiliki yote? Hawa watu wakuu wake Mungu wote wakubaliana kwamba ni kwa sababu sisi hatuelewi kwamba daraja la imani hufunga mwanya kati ya yale yote ambayo Mungu ametupa sisi pamoja na uweza wa kumiliki yale ambayo Mungu ametupatia sisi. Hii ndiyo sababu Mungu ametupatia sisi Kitabu cha Yoshua.

Katika Kitabu cha Yoshua twapata mifano kumi na sita ya imani. Wakati Mungu alipotutaka sisi kufahamu kuhusu imani katika kitabu cha Mwanzo, Yeye ametupatia sura kumi na mbili zinazotuambia sisi kuhusu huyu mtu Ibrahimu. Imani ni lazima iwe ni ya muhimu mno kwake Mungu kwa kuwa sababu ya kitabu chote cha Yoshua ni kutuonyesha sisi jinsi ya kuishi kwa imani, na kutembea kwa imani katika baraka zote za kiroho ambazo Yeye ametupatia sisi.

Kitabu cha Yoshua ni kuhusu Nchi ya Kanaani. Hii Nchi ya Kanaani itahamiwa ndani; itavamiwa mji mmoja kwa wakati mmoja, na taifa mmoja kwa wakati mmoja. Lakini ujumbe wa kiroho na wa ibada wake Yoshua siyo hasa kuhusu maeneo na pahala pa kijiographia, ni kuhusu kuzimiliki milki zako za kiroho kwa imani.

Nchi ya Kanaani ni picha ya makusudio ya wokovu wa taifa hili lao watu makhususi. Na kwa sababu neno "Wokovu" lamaanisha "Ukombozi", ukombozi wao kutoka Misri ni mfano wa wokovu. Wokovu wetu hutoka katika kuamini kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa pekee wake Mungu na mwokozi wetu wa pekee. Tunapoiweka imani yetu ndani Mwake, Yeye hutukomboa sisi kutoka kwa dhambi zetu, au kutoka "Misri yetu ya kiroho". Uvamizi wao pamoja na utekaji wa Kanaani ni picha ya udhamana wa maisha yake Mungu ambayo ameyafuma kwao watu wake ambao wameupata ujuzi wa wokovu kutoka mwelekeo wa "Misri" katika maisha yao.

Mtume Paulo atuambia sisi kwamba Mungu hutuokoa sisi kwa neema, kuipitia imani. Kulingana na Paulo, wokovu wetu siyo kwa sababu ya juhudi letu wenyewe. Ni kipawa chake Mungu, na siyo matokeo ya kazi yetu nzuri. Hata hivyo, Paulo pia aandika kwamba sisi tumeokolewa kwa kazi njema, ambazo Mungu ametuandalia kutoka hapo mwanzo kwa ajili yetu. Yeye atutaka sisi kutembea katika kazi hizo nzuri. Kazi hizo nzuri ni makusudio ya wokovu wetu <u>katika</u> <u>maisha</u> <u>haya</u> na ni sehemu ya "Nchi ya Ahadi" ya kiroho ambayo Mungu wetu anayetupenda sisi atutaka tuimiliki sisi – mita mraba mmoja kwa wakati mmoja.

Wokovu ni zaidi ya malipo ya njia moja hadi mbinguni. Ipo sababu ya wakati huu kwa wokovu wetu: "Kanaani" yetu ya kiroho hapa ulimwenguni. Sababu yasisi kutokurithi milki yetu ya kiroho yawezekana kwamba sisi hatufahamu jinsi ya kumiliki.

Hii ndiyo sababu Mungu ametupatia sisi kitabu cha Yoshua. Mungu ametupatia sisi kitabu hiki cha kwanza cha historia ya Agano La Kale ili iwe mfano kwetu sisi kuhusu dhamana ya imani ambayo kwayo twaweza kumiliki milki zetu za kiroho.

Sura ya Kumi na Moja

Maonyesho ya Imani

Kitabu cha Yoshua ni nakila ya uvamizi wa Nchi ya Kanaani. Tunapoisoma nakala hii, tutaona "Maonyesho ya Imani". Tunapokisoma Kitabu cha Yoshua, twapewa wazo njema kuhusu namna ya kumiliki baraka zetu za kiroho. Sura baada ya sura nyingine zatupatia sisi mifano na maonyo ambayo yatuonyesha sisi imani ni kitu gani na kile ambacho siyo imani. Sura hizi zitatandazwa na maonyo kuhusu hatari ya "Ulimwengu, Mwili, pamoja naye Shetani".

Kitu cha kwanza tunachokiona katika kitabu cha Yoshua ni kile ambacho twaweza kukitaja kama "Mabadiliko ya Imani". Tunayaona mabadiliko ya uongozi kutoka kwake Musa hadi kwake Yoshua tunaposoma hivi:

"Yoshua alikuwa amejawa na Roho, Kwa maana Musa alikuwa amemwekelea mikono juu yake. Kwa sababu hiyo watu wa Israeli wakamtii Yoshua jinsi ambavyyo walivyozifuata amri zake Bwana ambazo alikuwa amempatia Musa. Baada ya kifo cha Musa, mwanafunzi wake Bwana, Mungu alizungumza kwake Yoshua na kumwambia yeye, 'Musa mwanafunzi wangu amefariki. Wewe ndiwe kiongozi mpya wa Israeli. Waongoze watu wangu. Uwe mwenye nguvu na mwenye ujasiri, kwa kuwa wewe utakuwa kiongozi aliyefanikiwa kwao watu wangu. Wewe wahitajika kuwa mwenye ujasiri tu na kuitii kila sheria ambayo Musa alikupatia wewe. Kwa kuwa kama utakuwa mwangalifu kutii kila mmoja yake, wewe utafanikiwa katika kila kitu utakacho kitenda.

"Wakumbushe watu wakati wote kuhusu sheria hizi, nawe mwenyewe uzifikirie kila mchana na usiku ili uwe na uhakika kwamba utazitii. Na ni wakati huo tu utakapo fanikiwa. Uwe mwenye nguvu na mwenye ujasiri. Kumbuka Bwana Mungu wako yupo pamoja nawe po pote pale uendapo.'" (Yoshua 1:6-8)

Katika sura za kwanza za Kitabu cha Yoshua, twakiona kile ambacho twaweza kukitaja kama, "Fadhaha au bubuazi za imani". Tunapozidi kukua katika ufahamu wetu wa imani, yatubidi sisi tusifadhaishwe wakati tunapokumbana na shida ambazo hutuletea maswali ya changa moto kwa imani yetu. Ikiwa twaweza kuondoa shida zote na vizuizi vyote ambavyo huyaleta maswala haya yote ya imani, tutaondoa hitaji lenyewe la imani.

Huyu mwanamke Rahabu katika Yoshua sura ya pili atuletea shida na maswala kuhusu imani kwao watu wengi. Wapelezi wawili wa Kiyahudi walimtembelea kwake nyumbani na kujificha humo. Wakati mfalme wa Yeriko alipokuja kuwatafuta Wayahudi, yeye Rahabu aliwatorosha kwa njia nyingine. Mungu anambariki kwa sababu hii. twasoma katika sura kuu ya imani katika Bibilia kwamba huyu Rahabu alikuwa ni shujaa wa imani kwa kuwa alidanganya.

Kama ukitazama kwa ukaribu utaona kwamba huyu Rahabu hakutajwa kama mfano wa imani kwa kuwa alidanganya. Katika sura ya imani twasoma haya: "Kwa imani, kahaba Rahabu hakuangamizwa pamoja na wale ambao hawakuamini." Wakati wapelelezi wa Kiyahudi walipokuja katika nyumba yake, Rahabu alisema, "Mimi nafahamu kwamba nyinyi ni waakilishi wake Mungu wa kweli na anayeishi. Watu wengi hapa wanawaogopa nyinyi mno. Sisi twaamini kwamba Mungu yupo pamoja nanyi." (Yoshua 2:9)

Wapelelezi Waebrania wakafanya maagano pamoja naye na kuahidi kuyahifadhi maisha yake. Ni kwa sababu gani yeye aliokolewa? Imani yake ndiyo iliyomuokoa. Yeye

aliamini kwamba watu Waebrania walikuwa ni watu wake Mungu na kwamba Mungu wao alikuwa ni wa kweli na anayeishi. Rahabu alifanyika mmoja wa watu wake Mungu kwa kuwa alikuwa nayo imani.

Katika sura ya tatu utapata "Uthibitisho wa Imani". Wakati Mungu anapojaribu kutupatia sisi imani ili kuingia katika Kanaani ya kiroho, wakati mwingi ataidhibitisha imani yetu ili kututia moyo sisi. Twaliona jambo hili katika maisha yake Gidioni, ambaye aliiweka ngozi ya kondoo katika kuutafuta uthibitisho wake Mungu naye Mungu akauheshimu ule uthibitisho. Daudi atuambia sisi kwamba, "Hatua zake mtu huthibitishwa na Bwana." (Zaburi 37:23) Hii ya maanisha tunapozichukuwa hatua za imani, Mungu hubariki na kuthibitisha hatua hizo za imani.

Katika sura hii, Mungu alijithibitisha kwake Yoshua na kuwaonyesha watu kuwa baraka Yake ilikuwa juu ya kiongozi wao, Yoshua, kama ilivyokuwa juu yake Musa. Pia aliitenda miujiza hii kwa kuwatia nguvu ya imani watu. Kusudi la miujiza hii ilikuwa ni kuwaonyesha wao kwamba Mungu alikuwa pamoja nao, na wakati walipovamia miji iliyokuwa na ngome kuu ya Kanaani, kama vile Yeriko, Yeye angeliwabariki wao kwa ushindi.

Katika sura ya nne wana cha Israeli waliyajenga "Madhabahu ya Imani". Walipokuwa wakiuvuka mto wa Yordani, hata ingawa ulikuwa ni wakati wa mafuriko, maji yaligawanyika na wao wakavuka kama kwa nchi kavu. Walipokuwa wakivuka, waliamriwa kukijenga kinara kwa mawe, kwa ukumbusho wa muujiza huu mkuu ili wana wao wasisahau yale ambayo Mungu aliwatendea wao wakati walipokuwa nayo imani ya kuuvuka mto Yordani.

Katika sura ya tano twaona "Matakwa ya kwanza ya Imani". Kabla ya wana wa Israeli kuvamia Kanaani, wao walikuwa wameamriwa kumtahiri kila mwanamume miongoni mwao. Kizazi cha pili kilikuwa hakijatahiriwa. Kizazi cha kwanza, waweza kukumbuka, kiliangamia na kufa jangwani. Hii hadithi ya kuvutia ni mfano wa matakwa ya imani ya kweli. Kabla ya kuingia katika Nchi ya Ahadi ya baraka zake Mungu, ni lazima ujiulize mwenyewe ikiwa ipo dhambi ye yote katika maisha yako? Ipo dhambi ye yote katika maisha yako ambayo wahitajika kujitenganisha nayo mwenyewe?

Tulipokagua Kitabu cha Mwanzo, tulijifunza kwamba wengi miongoni mwao waamini hupita kando ya madhabahu haya ya toba ambayo Ibrahimu aliyajenga wakati maisha yake yalikuwa ni mfano wenye kujidhihirisha wa imani kwa ajili yetu. Wao hawajamruhusu Mungu kukumbana na dhambi katika maisha yao. Yatubidi kutubia dhambi iliopo maishani mwetu kabla ya kutarajia baraka yake Mungu juu ya maisha yetu. Hii ndiyo maana ya amri hii ya kuwatahirisha wanaume wote katika jumuia yote. Ni mfano wa kudhihirisha kwa nje kuhusu kule kujitolea kwa ndani kwa imani iliyo katika mioyo yetu. Maana ya kutahiriwa ambayo twaipata katika Agano La Kale yafanana mno na maana ya ubatizo tunaoupata katika Agano Jipya.

Katika Yoshua sura ya tano, utapata pia "Agizo la Imani". Hii yapatikana mwishoni mwa sura ya tano. Yoshua alikuwa ametoa maagizo kwamba hamna miongoni wa askari wake ambaye angeliutoa upanga wake. Jeshi likipiga kambi mashariki mwa Yordani katika giza kuu wangeliingiliwa na kuvamiwa nao maadui kwa urahisi mno. Na kwa sababu hiyo wakati mwingi wao walilitoa agizo, "Msiutoe upanga wenu ndani ya ala au mkoba wake." Kama wangelimuona mtu ye yote aliyeutoa upanga wake katika ala yake, wao wangelifahahu kuwa yeye alikuwa ni adui na kwa hivyo kukumbana naye kwa upesi iwezekanavyo.

Yoshua alitoka ili kutembea katika masaa ya usiku wa manane kabla ya vita ya Yeriko. Yeye alimuona mtu aliyeutoa upanga wake kwenye ala yake. Yoshua akamuuliza yeye, "Je! Wewe ni rafiki au adui?" Jibu lilikuwa, "Mimi ndimi Mkuu wa majeshi yake

Bwana!" Twasoma zaidi kwamba Yoshua alianguka chini mbele yake huyu mtu na kumuabudu Yeye na kusema, "Nipe mimi agizo lako." Mkuu wa majeshi akasema, "Vua viatu vyako, kwa kuwa mahala ulipo ni mahala patakatifu." Twazidi kusoma, "Naye Yoshua akatenda hivyo." (Yoshua 5:14-16)

Kulingana na sura ya sita ya Kitabu cha Yoshua, mpangilio wa vita ambao Yoshua aliupokea kutoka kwake Bwana usiku ule kabla ya vita ulikuwa kwamba taifa nzima la Israeli liliamriwa kutoka nje ya kambi yao, na kusafiri hadi katika kuta za mji, na halafu kuuzunguka mji wa Yeriko. Iliwabidi kufanya hivi kila siku kwa siku sita.

Katika siku ya saba waliambiwa kuuzunguka mji ule mara saba. Waliamriwa kuzunguka ule mji kwa mara kumi na tatu. Mji huu ulikuwa ukilindwa na kuta kuwa ambazo nyumba zilijengwa juu yake. Watu waliokuwa wakiilinda mji waliwaweka wanawake na watu wasiojiweza ambao hawangeliweza kuzibeba silaha juu ya kuta zile wakiwa nayo makaa ya moto, na mawe makubwa, au cho chote kile ambacho wangeliweza kukitupa juu ya vichwa vyao wenye kuwavamia.

Mmoja wa akida mkuu wa jeshi ambaye jina lake lilikuwa ni Abimeleki alitiwa aibu kwa kweli kwamba yeye alitembea karibu mno na kuta alipokuwa akiuvamia mji. Naye mwanamke ajusa akamwangushia jiwe kuu la kusagia juu ya kichwa chake. Akiwa kichwa chake kimepasuliwa, huyu Abimeleki akasema kwa mbeba silaha wake, "Uchukuwe upanga wangu na unidunge mimi, ili isije ikanenwa kwamba mwanamke ndiye alimuua Abimeleki." Waamuzi 9:52-54) Maneno haya yalikuwa ni yenye maonyo kwa Jeshi la Israeli: usisonglee karibu na kuta za mji. Kumbuka Abimeleki!

Hata hivyo Mungu alikuwa akimwaambia Yoshua kuwachukuwa watu wake wote karibu na kuta hizi kuu za mji wa Yeriko na kuzunguka mara kumi na tatu! Hii ilikuwa ndio mara ya kwanza yake Yoshua kuongoza vita na ni hakika kwamba angelitamani mno kama angelidhihirisha kipawa chake kama shabiki mwenye maarifa. Punde tu Yoshua atadhihirisha ushabiki na umaarufu wake kwamba yeye ni mwanajeshi mwenye umaarufu. Mpangilio huu wa vita ulikuwa ni wa kipumbavu mno na uliomfanya Yoshua kuonekana kama asiye nayo maarifa. Yoshua alitimiza kila agizo la mpango ule kwa kuwa alifahamu jambo mmoja kuuhusu mpango huu na ni kile ambacho alitakikana kufahamu kuuhusu mpango huu: *Ulikuwa ni mpango wake Mungu!*

Huku wakati wote walipokuwa wakiuzunguka ukuta wa Yeriko iliwabidi kuwa kimya. Watu wa mji wa Yeriko ni lazima kwamba walikuwa wamejawe na mshangao kwa kuwa wao hawakukirushia cho chote juu yao wana wa Israeli. Baada ya kuuzunguka ukuta ule kwa mara saba siku hiyo ya saba, Yoshua aliwageukia watu na kuwaagiza, "Pazeni sauti!"

Kitabu cha Waebrania cha sema kuta za Yeriko zilianguka chini kwa imani. Yoshua alikuwa mahala pa kuyaongoza makutano yao wana wa Israeli wote kuzizunguka kuta za Yeriko. Hili lilichukuwa imani. Ilichukuwa imani kwake yeye ili kudhihirisha kwao watu wale kila kitu kilichokuwa juu ya ukuta ule, mara moja kwa siku kwa siku sita, na halafu mara saba katika siku ya saba.

Vita vya Yeriko vyatuonyesha sisi namna ya imani ambayo hutufanya sisi kuingia katika "Nchi ya Ahadi", na kuishi kama watu wamchao Mungu. Namna ya imani hii ni yenye matendo. Hii ni imani inayo tembea. Imani ya Yoshua ambayo ilitembea kuzunguka Yeriko mara kumi na tatu siyo siri. Dhamana ya imani namna ile ni kutii. Imani ambayo "Hutembea" ni imani ambayo hutenda kazi. Imani ambayo iliyotembea na kutenda kazi siku ile ilikuwa ni imani iliyoshinda vita vya Yeriko kwake Yoshua nao watu wa Israeli. Namna ya imani ile yaweza kutenda kazi na kuvishinda vita vilivyomo maishani mwako siku ya leo.

Je! Imani yake ni ya namna ile? Baadhi yao watu wengine hufikiria kwamba imani haitakikani kuchukua hatua hadi wakati ambapo wao watakapoyaelewa mambo yote kwa mawazo yao. Lakini Yesu akawafundisha wafuasi Wake kujitolea wao wenyewe kwa tendo kwanza, naye akawaahidi kwamba uthibitisho wa kiakili utafuatia baadaye. Yeye alisema, "Ikiwa mtu ye yote atatenda, yeye atafahamu (Yohana 7:17). Kwanza, (katika kanunu), tembea kuzunguka Yeriko mara kumi na tatu, na halafu utavumbua imani inayofanya kazi na kushinda.

Mfalme Daudi aliandika katika Zaburi 27, "Ningalizimia kama nisingeliamini kuuona wema wake Mungu katika nchi yao walio hai." Watu wengine hufikiria kwamba "Kuona ndio kuamini", au kuona kutaongoza katika kuamini. Lakini Neno lake Mungu hutufundisha sisi kwamba kuamini hutuongoza katika kuona. Twauona huu mfumo wa agizo la imani likitajwa kwa fumbo lenye picha yake katika vita vya Yeriko.

Mungu angali akituchaji sisi kwa Mipango yake kwa maisha yetu. Wakati mwingine, uchaji wake kwa maisha yetu utaijaribu imani yetu wakati kama vile mpangilio wa vita vya Yeriko ulivyoijaribu imani yake Yoshua. Ikiwa wewe wamfahamu Mungu vyema, wafahamu kwamba uchaji wake hautakupeleka pale ambapo neema yake haiwezi kukulinda wewe. Kama wamfahamu Mungu anakuongoza kulitenda jambo fulani, lifanye. (Yohana 2:5). Kitabu cha Yoshua chatufundisha sisi kwamba imani ina matendo. Wakati inapotembea, hiyo hutenda kazi, na wakati ule inapotenda kazi, hiyo huvishinda vita vya maishani.

Sura ya Kumi Na Mbili

Maadui wa Imani

Baada ya kushindwa huko Ai, twasoma ya kwamba Yoshua aliangika chini kwa uso wake katika maombi ya bidii mno. Mungu akayajibu maombi yake Yoshua kwa kumuuliza Yoshua, "Mbona wanililia mimi? Israeli wamefanya dhambi!" tunapoziona ishara za utukufu kwamba Mungu yupo pamoja nasi, ishara hiyo hutupa sisi moyo katika kuendelea na imani yetu hukua wakati tunapofanya hivyo. Lakini, wakati ni wazi kwamba Mungu hayupo pamoja nasi, twahitajika kuwepo chini katika nyuso zetu hadi tutakapogundua sababu gani kwamba Mungu hayupo pamoja nasi. Mbona Mungu ayajibu maombi yake Yoshua kwa swali kama lile?

Katika Kitabu cha Kutoka, twasoma kwamba wana wa Israeli walikuwa migongoni mwao wamekaabiliana na Bahari ya Shamu na Jeshi la Misri lilikuwa likiwashambulia wao. Musa alauangusha chini uso wake mbele yake Mungu kwa maombi ya juhudi. Mungu akamuuliza Musa swali lile lile alilo muuliza Yoshua wakati alipomwangukia Mungu kwa uso wake katika maombi. Mungu akamwuliza Musa mbona alikuwa akiomba hali ilikuwa ni wazi kabisa kwamba angelizungumza nao watu wake Mungu ili wapate kuende mbele – hadi kwenye bahari!

Na kwa kuwa Yeriko ulikuwa ndio mji wa kwanza kuvamiwa huko Kanaani, sheria ya fungu la kumi iliwataka kwamba nyara zote kutoka katika mji wa kwanza kufanyika kuwa ni mali yake Bwana. Hamna sehemu ya nyara ile ingelifanyika kuwa ni mali yake mwanajeshi ye yote wa Israeli. Lakini ni wazi kabisa kwamba yupo mwanajeshi mmoja aliyechukuwa kitu huko Yeriko na kukificha. Mungu alimwambia Yoshua awapitishe mbele yake makabila kumi na mawili kwa ukaguzi. Wakati Mungu alipoonyesha kabila

lile liliokuwa na hatia, Mungu akaamuru kukaguliwa kwa kila mbari ya kabila lile lenye hatia. Mungu naye akaonyeshana jamii iliyokuwa na hatia. Kila jamii katika mbari ile ikakaguliwa mtu mmoja baada ya mtu mwingine hadi alipotajwa mtu aliyeitwa "Akani" aliyekuwa mwenye hatua. Yeye alikiri kuichukua dhahabu, fedha, pamoja na joho la mavazi kutoka Yeriko, ambayo alikuwa ameficha kwa kuzika chini ya hema lake. Yeye alihukumiwa na kufa papo papo.

Katika vitabu hivi vya kihistoria tumeshauriwa kuitizama mifano na maonyo (I Wakorintho 10:11). Kama jinsi ambavyo imani ya Yoshua ni mfano kwetu sisi wa kuigwa, pia kutokutii kwake Akani kwa hakika ni onyo kwetu la kutuhadharisha sisi. Wakati Mungu anapokiwekelea kidole chake juu ya dhambi iliyomo katika maisha yetu, twahitajika kuitilia mauti ile dhambi ili kwamba baraka yake Mungu ipate kurudi katika maishani mwetu (Wakolosai 3:5, 6; Warumi 8:13). Twaiona nidhamu ya kiroho mfano wake ukiwa katika maisha yake Akani.

Ulimwengu, Mwili, na Shetani

Na kwa sababu sisi tumeagizwa tusiupende ulimwengu au mambo yaliyomo katika ulimwengu, kwa karne nyingi watu wenye kumcha Mungu wameuona mfano wa ulimwengu katika ujuzi wake Akani huko Yeriko. Kushindwa kwao huko Ai kwafahamika kama mfano wa mwili. Yesu alifundisha: "Roho yataka lakini mwili ni mnyonge." (Mathayo 26:41) Mwili ni utu wa asili wake mwanadamu ambao hauna msaada wake Mungu. Kwa Kuwa mwili hutuletea kushindwa kwa kiroho chetu, kushindwa huku huko Ai kwaonekana kama mfano au fumbo kuhusu mwili. Ujuzi mwingine wa Israeli ulionakiliwa katika Kitabu cha Yoshua ni ule mfano ambao wawakilisha adui wa tatu wa imani, ambaye ni Shetani.

Wana wa Israeli sasa wakutana nao watu waitwao "Wagibioni". Na kama Rahabu, hawa Wagibioni walitambua kwamba watu wa Israeli walikuwa wakipitia Kanaani na kumwangamiza kila mtu. Wao walifahamu kwamba pia wao wataangamizwa na kwa sababu hiyo wao wakawadanganya wana wa Israeli. Wakavifanya viatu vyao kufanyika kuu kuu kwa kuvikwaruza katika miamba hadi vikaonekana kana kwamba vilikuwa vimevaliwa kwa miaka mingi na wakayafanya mavazi yao kuonekana kana kwamba yalikuwa ni makuu kuu mno. Hata ingawa wao walikuwa ni watu ambao walikuwa wakiishi katika nchi ambayo ilikuwa ikivamiwa, wao walijifanya kana kwamba wao walisafiri kutoka nchi ya mbali.

Wana wa Israeli wakaufanya mkataba pamoja nao hawa watu bila ya kumhusisha Mungu kwanza. Hawa Wagibioni wakawabembeleza wao kwa kusema, "Ufanyeni mkataba pamoja nasi. Sisi hatutoki katika nchi ya Kanaani. Sisi twatoka mbali mbali mno. Wao wakaingia katika mkataba na Wagibioni. Baada ya kuufanya mkataba, wana wa Israeli waligundua kwamba hawa Wagibioni hawakuwa wametoka katika nchi ya mbali, ila kwamba wao walikuwa ni wenyeji wa nchi ya Kanaani. Na kwa kuwa wao walikuwa wamekubaliana katika mkataba nao Wagibioni, kwa kuwa sababu waliochaguliwa walikuwa ni watu wenye stahi wao hawangelipata kuwaua wao. Waliwafanya watu waliowadanganya kufanyika kuwa watumwa wao Israeli.

Hawa Wagibioni wakamilisha mfano wa maadui wa imani katika Kitabu cha Yoshua. Adui wa kwanza wa imani yetu, ulimwengu, mfano wake ni Yeriko. Hadithi yake Akani ni mfano wa tamaa ya vitu vya ulimwengu huu. Katika njia ile ile aliyoitamani joho lile la mavazi, dhahabu pamoja na fedha, sisi hutamani mambo ya ulimwengu ambayo hutuvuta sisi kutoka kwake Mungu.

Kushidwa kwa Ai ni mfano wa mwili. Yesu alisema hivi, “Roho ataka, lakini mwili ni mdhaifu.” (Mathayo 26:40-42) Kwa kuwa wana wa Israeli hawakuchulia kwa uzito Ai, wao walishindwa huko Ai. Hadi walipo heshimu tisho lililotumainiwa kutoka huko Ai ndipo walipoweza kumshinda adui wao. Katika njia ile ile, sisi hupuzia kile ambacho Bibilia yakiita kama mwili wetu. Roho yaweza kushinda mwili wakati tunapotambua kwamba asili yetu ya kibinadamu bila ya usaidizi wake Mungu ni tisho kubwa kwa imani yetu. Usipuzie au kudharau uwezo uliopo katika mwili wako juu ya kutembea kwako kwa imani!

Wagibioni waliufanya mkataba wao kwa kuwahadaa Waisraeli. Shetani hutenda kazi kwa njia ile ile. Katika tenzi moja kuu, Martin Luther aliandika hivi kumhusu shetani, “ujanja wake pamoja na nguvu zake ni kubwa.” Shetani ni malaika wa nuru. (II Wakorintho 11:14) Yeye hatujaribu sisi kuanguka kwa kuyatenda mambo makubwa na maovu. Yeye hutujia sisi katika umbo la kitu chenye kupendeza, kitu chenye kuvutia. Ikiwa Mungu amekuita wewe kuwa ni Mmishonari Daktari, shetani hatakujaribu wewe kwa kuzivunja benki. Yeye atakujaribu kwa kufanyika daktari mzuri katika nchi yako. Yeye hutujia sisi katika umbo la kitu chenye kupendeza, kitu chenye kuvutia. Ikiwa Mungu amekuita wewe kuwa ni Mmishonari Daktari, huo ndio mpango bora wake Mungu kwetu sisi. Shetani hujaribu kutupata sisi katika kutenda yaliyo mema badala ya yale yaliyo bora. Hii ndiyo sababu wengine husema kwamba adui mkubwa wa kile kilicho bora ni kile kilicho kizuri. Yoshua sura ya sita hadi ile ya tisa hutupatia sisi picha ya hawa maadui watatu wa imani yetu: Ulimwengu, Mwili, na Shetani.

Pengine katika kitabu cha Yoshua, utayapata mafumbo mengine ambayo yaeleza tabia ya imani kwa ajili yetu. Maisha yake Yoshua, na mtu mwingine anayetajwa pamoja na Yoshua, hutupatia sisi, “Maelezo ya tabia bora ya Imani”. Mmojawapo wao watu wakuu wa imani katika Bibilia ni Kalebu. Yeye alikuwa ndiye mmojawapo kati ya mpelelezi yule mwingine ambaye aliyeileta habari njema pamoja na Yoshua. Kalebu hakuyapoteza maono yake. Nyakati zote walizokuwa wakizunguka huko jangwani wakiwaona watu wakinung’unika na kufa kwa kiu, kalebu aliendelea kufikiria kuhusu tende ambazo alizoziona wakati yeye pamoja na Yoshua walikuwa ni wapelelezi katika mji wa Hebroni.

Wapelelezi wale wengine kumi walikuwa ni watu stadi na bingwa katika elimu ya “Majitu” – kutilia mkazo shida, au majitu, kama tulivyo sema wakati tulipokisoma kitabu cha Hesabu. Kalebu aliwaona majitu, lakini alifahamu Mungu wake alikuwa ni mkubwa kuwaliko wale majitu. Walipofika katika Nchi ya Kanaani, Kalebu alivamia na kumiliki mji wa Hebroni, ambao alikuwa ameahidiwa na Musa.

Yapo tena “Maelezo yaliyo ya kinyume ya Imani” Katika Kitabu cha Yoshua. Pamoja na wale wapelelezi kumi ambao hawakuwa nayo imani hata kidogo, kweli kwamba wana wa Israeli walishindwa kuyavamia mataifa yote ya Kanaani kama jinsi ambavyo Mungu alikuwa amewaagiza wao kutenda, ni maonyesho yaliyo ya kinyume ya imani. Ikiwa walikuwa wameutimiza mpango wake Mungu, hatungeliweza kusoma katika kitabu kifuatacho cha Bibilia kwamba wao walifanywa kuwa watumwa kwa nyakati saba na mataifa yale waliyoshindwa kuyavamia na kuyateka.

Picha ya mwisho ya imani ambayo twaipata katika Kitabu cha Yoshua yaweza kuitwa “Kukata kauli ya Imani.” Yoshua aliwapa changa moto watu wake kuiweka mihuri imani ya kuwa kufanya agano na Mungu. Akiwaonyesha mfano wake, yeye alisema, “Kwangu mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana.” (Yoshua 24:15) Yoshua aliweka mhuri imani yake kwa agano. Alifanya ijulikane kwamba yeye pamoja na nyumba yake watamweka Mungu kwanza na kumtumikia. Wakati Yoshua alipowapa changa moto watu wake kuungana katika kulifanya agano la namna ile, wao walitenda hivyo, wakisema,

“Tumechagua kumtumikia Mungu na kumfanya Yeye awe wa Kwanza.” Yoshua alinakiliwa akisema, “Mungu ndiye shahidi kwa hili na pia nyinyi ni mashahidi kwa hili. Mumefanya agano siku ya leo kwamba mtamweka Mungu kwanza na kutaka kumtumikia yeye.” (Yoshua 24:14-16)

Kitabu cha Yoshua cha malizia na Yoshua akiwaagiza watu wake Mungu jinsi ambavyo Musa alivyofanya mwishoni mwa vitabu vya Kumbu Kumbu La Torati na Walawi. Musa na Yoshua watupa sisi changa moto kuleta mambo ya imani katika kuikata kauli ya kujitolea kumfanya Mungu kuwa wa kwanza katika maisha yetu.

Je! Umewahi kuyaleta mambo ya imani na kuikata kauli na kujitolea kabisa kwa imani kwake Mungu? Je! Umeufanya uamuzi katika moyo wako kwamba wewe na jamii yako mtamweka Mungu kwanza na kumtumikia Mungu mmoja wa pekee na wa kweli? Kusanya pamoja maelezo ya tabia ya imani katika Kitabu cha historia chenye Uvuvio kilichoko katika Agano la Kale. Kwa uangalifu hebu tafakari jinsi ambavyo kitabu hiki cha imani kinavyo malizika. Halafu, mpe Roho Mtakatifu ruhusa kukuongoza wewe katika kujitolea na kudhibitisha agano lenye namna ya imani ambayo umeiona imeelezwa katika Kitabu cha Yoshua.